AMBOLA

SEASON 04

PALE MASHUJAA WANAPOLISALITI TAIFA LAO

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

HADITHI HII NI YA KUBUNI HAINA MAHUSIANO NA TUKIO LOLOTE LA KWELI.

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

SIMULIZI ZA MAPENZI

1.MISS TANZANIA
2.SERENA
3.BEFORE I DIE
4.BEYOND PAIN

SIMULIZI ZA UPELELEZI

5.PENIELA
6.QUEEN MONICA
7.THE FOOTBALL
8.I DIED TO SAVE PRESIDENT
9.KIAPO CHA JASUSI
10.KIKOSI CHA SIRI
11.SIRI
12.SCANDAL(KASHFA)
13.CAPTURE OR KILL MISSION
14.JAMII YA SIRI

MAWASILIANO
0764294499

© 2020 Masimulizi.Haki zote zimehifadhiwa

KITABU HIKI TAYARI KIPO MTAANI



WASILIANA NA MAWAKALA WAFUATAO KUKIPATA KITABU HIKI

DAR ES SALAAM - 0678683278 , 0653254110

IRINGA - 0755028070

MUSOMA - 0755993326

DODOMA - 0768109159

MWANZA - 0735475112

ARUSHA - 0757690302

MBEYA - 0755501100

KIGOMA - 0763317569

MIKOA MINGINE WASILIANA NA 0764294499

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Sasa kazi inaanza rasmi.” Alisema Mathew

“Tunaanzia wapi? Aliuliza Ruby

“Tunaanza kwa kuwachunguza viongozi wa chama cha ukombozi wa Afrika.Regina alituambia kwamba Amani ambaye aliuawa alikuwa anamchunguza mwenyekiti wa chama cha ukombozi.Tunaanza na sisi kumchunguza mwenyekiti

huyo.Tutawachunguza pia viongozi wengine wa juu wa chama hicho ambao wanazifahamu siri za chama.Hatutasahau kumchunguza pia mgombea wao wa uraisi kumfahamu ni nani.Wakati huo huo tutajielekeza pia katika kumtafuta Gosu Gosu na ili tujue mahali alipo Gosu Gosu tutalazimika kujua kwanza mahali alipo Ambola.Mwanamke yule kuna kitu anakifahamu kuhusu suala la Gosu Gosu" alisema

Mathew na kuinuka akaenda kumchukua Regina.

“Regina nimekuleta hapa kuna mambo tunahitaji utusaidie .Leo tunaianza rasmi kazi yetu ya uchunguzi kubaini mipango ya hujuma katika uchaguzi mkuu.Ulituambia Amani alikuwa anamchunguza mwenyekiti wenu lakini kwa bahati mbaya aliuawa kabla ya kukupa kile alichokipata katika uchunguzi wake.Tunaanza kumchunguza huyo mwenyekiti wa chama.Tunaomba kumfahamu

jina lake,namba yake ya simu kama unaikumbuka,aina ya gari analoendesha,kinywaji anachotumia,rangi anayoipenda.Hali yake ya ndoa nikimanisha ana mke na watoto wangapi? Wako wapi? Ana kimada? Tunataka kufahamu mambo kama hayo.” Alisema Mathew.

“Inaonesha hamjalala usiku wa leo” alisema Regina

“Tutalala pale tutakapohakikisha nchi ni salama.Tusipoteze muda

tafadhali tupe taarifa” alisema Mathew.

“Mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika anaitwa Israel Maungwana.Umri sifahamu ana miaka mingapi.Namba yake ya simu sijaiweka kichwani.Kwa ufupi tu ni kwamba mimi si mtu wa karibu sana na mwenyekiti huyo wa chama.Mahusiano yetu ni ya kikazi.Makutano yetu ni katika vikao vya kazi hivyo sijapata wasaa wa

kufahamu mambo yake mengi.” Alisema Regina

Wakati Regina akitoa maelezo yake,Ruby alikuwa anaandika haraka haraka katika kompyuta yake na mara Regina akaiona picha katika runinga iliyokuwa ukutani.

“That’s him.Yule ndiye mwenyekiti wa chama” alisema Regina.Mathew aliinuka akaisogelea runinga ili aitazame vizuri ile picha.

“I know this guy.” Alisema Mathew

“You know him? Aliuliza ruby

“Yes.I know him” alijibu Mathew na kumgeukia Regina.

“Una hakika huyu ndiye mwenyekiti wa chama? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo.Huyu ndiye Israel Maungwana mwenyekiti wa chama cha Ukombozi wa Afrika” alisema Regina.

“Mathew umeshtuka baada ya kumuona huyu mtu.Who is he? Aliuliza Ruby.Bado Mathew alikuwa

amesimama akiitazama ile picha runingani.

“Mathew ! aliita Ruby.

“Ni nani huyu mtu? Aliuliza Ruby”

“Jina lake siyo Israel Maungwana.This man is very very dangerous .” Alisema Mathew akiwa bado amesimama akiitazama ile picha ya mwenyekiti.

“Hapa kuna kazi kubwa.Huyu mtu ni hatari mno zaidi ya mnavyofikiria” alisema tena Mathew.

“Tuambie tafadhali ni nani huyu mtu? Aliuliza Ruby

Mathew alienda kuketi katika kiti.Bado aliendelea kuitazama ile picha halafu akavuta pumzi ndefu.

“Toka nimemfahamu Mathew Mulumbi ni mara ya kwanza ninamuona akiitazama picha ya mtu namna hii.Ni mara kwanza amerudia mara mbili kutamka kuwa mtu huyu ni hatari.Ni mara ya kwanza Mathew ameonesha hofu.Haijawahi kutokea hata mara moja.Huyu mtu lazima

ni hatari zaidi ya ziraili mtoa roho” aliwaza Ruby.

ENDELEA……

AMBOLA

Uliwadia muda wa kurejea nyumbani. Wanafunzi walitoka madarasani baada ya kengele kugongwa na kuelekea sehemu ya maegesho ya magari kulikokuwa na mabasi ya shule kwa ajili ya kuwapeleka wanafunzi sehemu mbali mbali wanazotoka.

Ambola aliagana na wanafunzi wenzake waliopanda basi la shule, akaelekea katika sehemu yanakoegeshwa magari ya wageni.Ambola ni mmoja wa wanafunzi ambaye hutumia gari binafsi kwenda na kurudi shuleni. Alipofika katika maegesho ambako alitegemea kumkuta dereva wake, alishangazwa na kile alichokikuta. Alimkuta baba yake akiwa amesimama nje ya gari akizungumza na simu. Alishangaa.

“Baba! Alisema Ambola kwa mshangao uliochanganyika na furaha. Baba yake alikata simu akampokea begi halafu akamfungulia mlango.

“Baba sikutegemea kabisa kukuona hapa leo. Uncle Samwel ana matatizo? Aliuliza Ambola

“Nilimpigia simu nikamtaka leo apumzike nimekuja kukuchukua mimi mwenyewe. Hujafurahi? aliuliza baba yake Ambola

“Nimefurahi sana baba.” alijibu Ambola huku akiingia garini.

“Masomo yanakwendaje? Aliuliza baba yake Ambola wakati wakitoka katika geti la shule ile ya kimataifa.

“Masomo yanakwenda vizuri. Tumepata waalimu wapya wa Sayansi kutoka nchini Japan.” Alijibu Ambola

“Vizuri sana’ alisema Julius Kabombe baba yake Ambola. Ukimya mfupi ulitawala hadi walipoingia katika barabara kuu.

Walisimama kwa dakika kadhaa katika foleni. Wakiwa katika foleni ile walitokea watoto wawili wakagonga dirisha na kuonesha ishara ya kuomba msaada. Baba yake Ambola alitoa pochi yake akatoa noti mbili za elfu kumi akampatia Ambola.

“Wape watoto wenzako. Wana mahitaji”

Ambola alishusha kioo cha dirisha, akawapatia watoto wale kila mmoja noti moja.

“Baba kwa nini watoto hawa wanaomba mitaani?

Hawasomi? Aliuliza Ambola na wakati huo tayari gari zilianza kwenda. Zilipita dakika kadhaa bila baba yake kutoa jibu.

“Baba nimekuuliza kwa nini watoto wale ambao wana umri wa kwenda shule wapo barabarani wakiomba? Wazazi wao wako wapi? Aliuliza Ambola

“Ambola kuna mambo ambayo kwa umri wako ni vigumu kuyaelewa.” Alijibu baba yake

“Nimekuuliza kwa sababu ninataka kuelewa. Kwa nini kila siku watoto hawa wako mtaani? Kwa nini watu wanaomba msaada barabarani? Kwa nini wanakosa chakula? Kwa nini wanakosa hela ya kutumia? Wakikosa barabarani wanaishi vipi? Aliuliza Ambola

“Ambola maswali yako yanahitaji majibu marefu lakini ninakuahidi nitakujibu maswali yako baadaye. Kwa sasa nataka nikukumbushe tu kuwa kamwe usibweteke kwa

utajiri mdogo nilionao baba yako. Utajiri huu unaweza ukayeyuka kama barafu ndani ya muda mfupi. Utajiri pekee ambao hauwezi kupotea ni elimu. Jitajhidi sana kusoma kwa bidii. Watoto kama wale wanaoomba barabarani si kwamba wanapenda, lakini imewalazimu kufanya hivyo kutokana na hali ngumu ya maisha inayowakabili. Nimekupeleka katika shule bora kabisa ili ujifunze mambo mengi, hivyo usifanye mchezo na elimu hata kidogo. Umenielewa Ambola?

“Nimekuelewa baba. Nitasoma sana hadi nitimize ndoto zangu. Sitaki kuwa masikini” Alisema Ambola

“Nafurahi kusikia hivyo. Narudia kukusisitiza hata kama ikitokea Mungu akanichukua leo kamwe usirudi nyuma. Mng’ang’anie sana elimu.” Alisema baba yake Ambola.

“Baba usiongelee masuala hayo ya kufa tafadhali.” Alisema Ambola.

“Ambola kifo kipo. Sisi sote tutakufa hilo lazima

tulikubali. Hata hivyo dhumuni lingine la kuja kukuchukua mimi mwenyewe ninataka tupite katika kaburi la mama yako. Kama angekuwa hai, kesho tungesherehekea kumbu kumbu ya siku yake ya kuzaliwa.” Alisema Julius.

“Ninasikitika sana sikuwahi kumuona mama yangu.” Alisema Ambola halafu akafungua mkebe wake wa kuhifadhia kalamu.Ndani ya mkebe ule kulikuwa na picha ya mama yake

akitabasamu. Aliitazama kwa muda picha ile hafalu akatabasamu na kusema.

“Laiti ningemuona Mungu, ningemuomba anirejeshee mama yangu japo kwa siku moja tu nimuone nizungumze naye.” Alisema Ambola halafu akamgeukia baba yake.

“Japokuwa sijawahi kupata malezi ya mama, lakini baba ninakusifu kwa kuwa umejitahidi sana kuziba pengo lake. Umenifanya nimekuwa na furaha wakati mwingine kuzidi hata watoto wenye

wazazi wao wote wawili. Ahsante sana baba” alisema Ambola

“Ni jukumu langu kuhakikisha unakuwa na furaha muda wote” alisema Julius Kabembo.

“Baba kwa nini baada ya mama kufariki hukutaka kuoa mke mwingine? Aliuliza Ambola. Baba yake alitabasamu na kuuliza.

‘Unataka nitafute mwanamke nioe? Aliuliza

“Kwani huruhusiwi kuoa tena? Ambola naye aliuliza

“Ninaruhusiwa”

“Kwa nini hutaki kuoa tena kama unaruhusiwa? Aliuliza Ambola

“Ambola umeuliza swali kubwa ambalo majibu yake hayaendani na umri wako. Hata hivyo kukujibu kwa kifupi ni kwamba sitaki kuoa kwa sababu mwanamke mwingine anaweza kukutesa. Mimi niliwahi kulelewa na mama wa kambo ninafahamu mateso niliyoyapitia. Sitaki

yale niliyopitia mimi na wewe uyapitie ndiyo maana baada ya mama yako kufariki sikutaka kuoa tena mwanamke mwingine. Lakini fahamu kuwa si mama wote wa kambo ni wabaya" Alijibu Julius.

"Ahsante sana baba kwa kunijali" alisema Ambola na safari ikaendelea kimya kimya hadi walipofika katika makaburi ya Jiwe barafu. Walishuka garini wakaingia ndani ya makaburi. Ambola alionesha woga sana lakini baba yake alimshika mkono na

kumtaka asihofu. Walifika katika kaburi la mama yake Ambola. Kila mmoja aliweka shada la maua. Julius aliongoza sala fupi kumuombea marehemu. Baada ya sala ile fupi Julius aliketi juu ya kaburi akamtaka Ambola naye aketi.

“Hapa ndipo alipopumzishwa mama yako. Ni mwanamke ambaye sikuwahi kuona mzuri zaidi yake duniani lakini aliniacha wakati ambao ninamuhitaji sana. Hata hivyo aliniachia

zawadi ya malaika ambaye naye ni mzuri kama yeye” alisema Julius na kumtazama Ambola wote wakatabasamu. Walikaa mahali pale kwa nusu saa halafu wakaondoka.

“Ambola kuna sehemu nyingine nataka nikupeleke kabla hatujarudi nyumbani lakini kabla ya kwenda huko, nataka tupite kwanza madukani uchague kitu chochote unachokitaka” alisema Julius.

“Nina kila kitu ninachohitaji baba sihitaji tena kitu kingine” alisema Ambola

“Ambola huwezi kuwa na kila kitu. Nitakupeleka dukani utachagua kila unachokihitaji nitakununulia” alisema Julius.

Walikwenda katika maduka kadhaa ambako Ambola alichukua kila kilichompendeza. Baada ya manunuzi walielekea mahali ambako Julius alitaka wapite kabla ya kwenda nyumbani kwao.

****

Kwa kutumia kitanza mbali, Julius alifungua geti baada ya kufika katika nyumba iliyozungukwa na ukuta wenye rangi nyeupe. Ukuta ule ulikuwa mrefu na mtu ukiwa nje unachoweza kukishuhudia kutokea ndani ni bati jekundu la nyumba iliyo ndani. Baada ya kuingia ndani geti lilijifunga. Julius aliegesha gari katika banda maalum kwa ajili ya kuegeshea gari.

“Tushuke” Julius alimwambia Ambola ambaye alifungua mlango akashuka.

“Hapa ni wapi? Aliuliza Ambola akionekana kuyafurahia mazingira mazuri ndani ya nyumba ile. Julius alitoa kadi katika pochi yake ndogo akaelekea mlangoni akaipitisha katika kifaa Fulani chenye namba pembeni ya mlango, halafu akakiminya kitasa mlango ukafunguka. Ambola alimfuata baba yake wakaingia ndani.

“Nyumba nzuri sana hii. Nani wanaishi hapa? Aliuliza Ambola akitabasamu baada ya kuingia katika sebule nzuri iliyosheheni samani za kupendeza.

“Ambola hii ni nyumba yako.” Alisema Julius na kutabasamu baada ya kuliona tabasamu pana usoni kwa binti yake.

“Hii ni ya kwangu? Ambola alishangaa.

“Ndiyo, hii ni nyumba yako. Sikutaka kukwambia kama nimekujengea nyumba.

Nilikuwa nasubiri utakapomaliza shule ndipo nikukabidhi. Hata hivyo nimeona leo nikwambie ukweli kuhusu nyumba hii kwani mambo ya Mungu ni mengi. Hakuna anaye ijua kesho yake ndiyo maana nimeona ni vyema nikakufahamisha kuhusu uwepo wa nyumba hii.” Alisema Julius na kufungua moja ya kabati lililokuwapo pale sebuleni, akatoa ramani ya nyumba ile akamuonesha Ambola.

“Nyumba hii ina vyumba vitatu vya kulala kila kimoja kikiwa kimejitosheleza kila kitu ndani. ” Alisema Julius akimuelekeza Ambola kuhusiana na nyumba ile. Alimzungusha kuona sehemu mbali mbali za ile nyumba. Ambola alifurahi sana. Nyumba ilikuwa nzuri mno iliyokuwa na kila kitu alichokipenda.

“Baba ahsante sana.Umenifurahisha mno. Sikutegemea kama siku moja na mimi nitakuwa na nyumba

nzuri kiasi hiki” alisema Ambola.

“Chumba cha mwisho ambacho nataka kukuonesha ni chumba cha mapumziko” alisema Julius huku akiufungua mlango wa chumba cha mapumziko kwa kutumia kadi.

“Hiki ndicho chumba maalum kwa ajili ya kupumzika pale unapokuwa umechoka. ” Alisema Julius na kubonyeza kitanza mbali kilichokuwa juu ya meza, maji yakaanza kushuka katika

mawe yaliyokuwa yamepangwa kitaalamu sana na kutengeneza maporomoko ya maji.

“Wow ! waterfall” alisema Ambola kwa furaha.

“Ninafahamu unapenda nini ndiyo maana nikajitahidi kuhakikisha kila unachokipenda kinapatikana ndani ya nyumba yako. Laiti ningepata eneo kubwa ningeweza kukuwekea hadi bustani ya wanyama lakini eneo ni dogo” alisema Julius. Kwa furaha aliyokuwa nayo

Ambola alikwenda kumkumbatia baba yake.

“Ahsante sana baba. Umenifurahisha mno” alisema Ambola.

“Usijali. Sasa naomba uketi katika lile sofa pale halafu utazame ukutani” alielekeza Julius. Ambola aliketi katika sofa aliloelekezwa.

“Unaona nini ukutani? Aliuliza Julius.

“Ninaona ramani tatu” alijibu Ambola.

“Vizuri sana.Ukutani kuna ramani tatu. Moja ramani ya Tanzania, inayofuata ni ramani ya Afrika na ya mwisho ni ramani ya dunia.” Alisema Julius akanyamaza kwa muda akizitazama ramani zile.

“Umejiuliza kwa nini nimekuwekea ramani hizi tatu na si picha za wanyama au wanamuziki uwapendao? Aliuliza Julius

“Nadhani ni moja ya urembo” alijibu Ambola.Baba yake alitoa kicheko kidogo.

“Ambola huu si urembo. Ramani hizi zina maana kubwa sana ndiyo maana nimeziweka humu. Hizi si ramani zile ambazo umezoea kuziona shuleni zikionesha mipaka, miji n.k. Hizi ni ramani maalum kabisa ambazo huwezi kuzipata sehemu yoyote” alisema Julius akazitazama tena zile ramani halafu akamtazama Ambola.

“Japokuwa umri wako bado mdogo lakini ninataka kukufahamisha jambo moja. Ramani hizi ni ramani za siri

sana kuhusiana na utajiri wa madini katika kila nchi duniani.” Alisema Julius.

“Wewe umezipata wapi baba? Aliuliza Ambola.

“Kama nilivyokwambia kuna mambo mengine ni makubwa kuzidi umri wako. Utafahamu baadaye utakapokuwa mkubwa lakini kwa sasa naomba nikueleze kwa nini ramani hizi ziko humu ndani” alinyamaza kidogo akazitazama tena ramani zile kwa umakini mkubwa halafu akasema.

“Tukiwa njiani, uliwaona wale watoto waliokuwa wakiomba msaada barabarani ukauliza kwa nini wanaomba? Nilikwambia nitakujibu baadaye.” Alisema Julius halafu akaitazama tena ile ramani ya Tanzania.

“Ukitazama ramani hii ya Tanzania imejaa rangi za aina mbali mbali. Rangi hizo zote zinaonesha aina mbali mbali za madini yanayopatikana hapa Tanzania. Ramani hii ilitengenezwa kwa siri kubwa na mabeberu. Nchi yetu

ilifichwa kuhusiana na ramani hii Lengo la kuificha ramani hii ni ili watanzania wasifahamu kuhusu utajiri mkubwa walionao.” alisema Julius na kunyamaza baada ya Ambola kuonesha anataka kusema kitu.

“Hao mabeberu ni akina nani? Nifahamuvyo mimi beberu ni dume la Mbuzi.”

“Ndiyo maana nikakwambia kuwa mambo mengine ni makubwa kushinda umri wako ila nitajaribu kukuelezea. Beberu

ni neno ambalo tunalitumia kuwaita waporaji wa mali za nchi yetu. Sina hakika kama ni neno rasmi lakini tunalitumia sana katika maana hiyo niliyokwambia. Beberu yaweza kuwa nchi, mtu au kikundi cha watu. Imezoeleka kwamba mabeberu ni wazungu lakini wapo pia mabeberu waafrika na hata mabeberu watanzania. Afrika imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi mno hivyo hawa watu ambao tunawaita mabeberu wanatumia kila mbinu kuhakikisha wanachukua mali hizo kwa

ajili ya kujinufaisha wao na nchi zao.” Alisema Julius.

“Mabeberu ni wakoloni? Ambola aliuliza.

“Ni wale wale. Mwanzoni walikuja wakatutawala, wakatudhalilisha, wakabeba mali zetu wakazitajirisha nchi zao huku sisi wakituachia umasikini mkubwa. Kwa jitihada za wazee wetu akina mzee Nyerere na wenzake mnaowasoma katika historia, walifanikiwa kuwaondosha wakoloni barani Afrika.Hadi leo hii bara zima la Afrika liko

huru. Pamoja na kufanikiwa kuwaondoa wakoloni hao barani Afrika, lakini wanarudi kwa namna nyingine na kuendelea kuufaidi utajiri wetu. Ndio hawa tunaowaita mabeberu.” alisema Julius.

“Kwa maneno mengine tunaweza kuwaita mabeberu ni wezi wa mali zetu” alisema Ambola.

“Tunaweza kuwaita hivyo kwa sababu wanachokihitaji ni kujinufaisha wao na nchi zao kwa kutumia rasilimali zetu. Hawatupendi, hawapendi nchi

zetu wanachokipenda ni mali zetu. Watu hao, wako tayari kuwafarakanisha waafrika wapigane wenyewe kwa wenyewe ili wapate nafasi ya kupenya na kupora mali.” alisema Julius.

“Hakuna sehemu ya kuwashitaki hao mabeberu wanaoiba mali zetu? Kuiba ni kosa na zipo adhabu kwa wezi. Kama watu wanaoiba mali za watu wengine wanafungwa gerezani kwa nini hao mabebeu wasishitakiwe nao kwa kuiba mali zetu? Aliuliza

Ambola. Julius alitabasamu kisha akasema.

“Hawa ni watu wakubwa. Wanaitawala dunia. Wameshika kila kitu hadi uchumi wetu. Tunawategemea wao kwa kila kitu. Tunazo rasilimali nyingi kama madini lakini bado hatuna uwezo wa kuyachimba tunawategemea wao. Wanachimba kisha wanatupangia bei ya kuuza na wanatupangia hadi kiasi cha kutupa kutokana na mali yetu wenyewe. Tunalima mazao mengi lakini hatuwezi kupanga

bei katika soko la dunia. Wanatupangia tuuze bei gani mazao yetu. Hakuna sehemu ya kuwashitaji hawa wakubwa. Wameishika Afrika wanaigeuza wakavyo.” Alisema Julius .

“Lakini baba tutawaacha watu hawa hadi lini waendelee kutuibia mali zetu? Hadi lini tutaendelea kuwa masikini wakati tunao utajiri mkubwa kama unavyosema? Aliuliza Ambola.

“Swali lako linaturejesha katika ramani hii. Ukitazama

utaona kuna rangi mbali mbali karibu kila sehemu ya nchi yetu. Hizi rangi zote ni madini na rasilimali nyinginezo ambazo zinapatikana hapa nchini kwetu. Wenzetu hawa kwa kuwa tayari wamepiga hatua kubwa kiteknolojia wameweza kufanya utafiti wao wakagundua kila aina ya madini yanayopatikana hapa nchini kwetu, wakatengeneza ramani hii ambayo haijawahi kuwekwa wazi. Ilifichwa ili watanzania wasifahamu uwepo wa utajiri mkubwa katika nchi yao. Tunafahamu uwepo wa

madini kadhaa makubwa kama Dhahabu, Almasi, Tanzanite n.k lakini kuna mengine yapo makubwa na ya thamani kubwa ila hayatajwi. Yote yapo katika ramani hii. Wakubwa hawa waliotengeneza ramani hii, wanataka kushirikiana na watu wetu waliokosa uzalendo kupanga mikakati ya kuja kupora madini hayo ambayo tumefichwa tusiyafahamu. Katika jambo hili hata viongozi wa serikali wanahusika” Alinyamaza Julius na kumtazama mwanae.

“Ambola jambo hili ni kubwa na kama nikiendelea kukueleza litazidi kukuchanganya. Ninaomba nijibu swali lako kuhusiana na umasikini wetu. Hawa tunaowaita mabeberu ndio waliotusababishia umasikini mkubwa wakishirikiana na watu wa ndani ya nchi zetu. Wao ni sababu ya kuwaona watoto kama wale wakiomba barabarani. Laiti kama rasilimali zetu zingekuwa zinatunufaisha kusingekuwa na watoto ambao wana umri wa kwenda shule lakini

wanashinda barabarani wakiomba msaada. Mabeberu ni watu wa kuwachukia mno. Nimeamua kukupa picha japo kidogo ya kile kinachoendelea hapa nchini kwetu na bara la Afrika kwa ujumla. ”alisema Julius na Ambola akasimama akaisogelea ile ramani.

“Baba kwani sisi si taifa huru? Kwa nini bado hao mabeberu wanaendelea kuja kuchukua mali zetu? Aliuliza Ambola

“Ambola sisi ni taifa huru lakini hatuko huru kiuchumi.

Uhuru wa kweli ni uchumi. Itoshe tu kwa haya niliyokwambia kwani nikiendelea zaidi nitakuchanganya” alisema Julius

“Baba, nimesoma historia tuliwahi kupigana vita na nchi ya Uganda tukashinda kwa kutumia majeshi yetu. Kwa nini tusitumie majeshi yetu kuwaondoa hao mabeberu? Aliuliza Ambola.

“Ambola hii si vita ya kubeba silaha na kuingia msituni kupigana. Hii inaitwa

vita ya kiuchumi. Ni vita ngumu kuliko hata vita ya silaha. Kwetu sisi silaha yetu kuu ambayo tunaweza kuitumia katika mapambano haya ni umoja wetu na mshikamano. Mabeberu hawa ili kutimiza malengo yao lazima kwanza wawavuruge msiwe wamoja.
Wanapandikiza chuki miongoni mwenu na mkianza kuchukiana, kupigina, mkiuana ndipo wao hupata nafasi ya kupenya kati kati wakachukua kile wakitakacho.
Imetosha kwa leo

nitakufundisha zaidi siku nyingine kama Mungu akitujaalia uhai" alisema Julius.

'Baba nina hamu sana ya kutaka kufahamu kuhusu hao mabeberu ambao wanabeba mali zetu" alisema Ambola.

"Siku nyingine nitakueleza zaidi lakini ninachotaka kukwambia ni kwamba hata kama ikitokea leo nikaaga dunia usiache kusoma. Soma kwa bidii na siku zote uwe na malengo ya kuja kuikomboa jamii yetu masikini kutoka

katika makucha ya mabeberu. Yawezekana usirejee tena katika nyumba hii hivi karibuni lakini naomba usimueleze mtu yeyote kuhusiana na ramani hizi nilizokuonesha. Ni kitu cha hatari sana na cha hatari kubwa. Utakapokuwa mkubwa utakuta nimekuwekea maelekezo yote katika kasiki hili hapa. Nitakupa namba za kufungulia kasiki hili uziweke kichwani na humu ndimo zinamokaa ramani. ” Alisema Julius huku akizitoa ramani

zile ukutani akazikunja na kuziingiza katika kasiki.

“Nani anaishi hapa katika hii nyumba? Aliuliza Ambola.

“Kuna mtu ambaye nimemjengea nyumba ya kuishi hapo pembeni ya nyumba hii anaitwa Mustapha.Yeye ndiye mlinzi wa nyumba hii. Pamoja na kulinda pia hufanya usafi kuzunguka nyumba na kuhakikisha mazingira yanakuwa safi muda wote.” Alisema Julius akamshika

mkono mwanae wakaenda kuketi sofani.

“Ambola hiki ulichokishuhudia ni siri kubwa sana ambayo hukupaswa kuifahamu. Imenilazimu kukuambia siri hii kwa ajili ya tahadhari. Leo ama kesho ninaweza kupoteza maisha hivyo kama nataka ufahamu namna nchi yetu na bara la Afrika tunavyoibiwa mali zetu. Lengo langu ni kutaka watanzania wafahamu ukweli kuhusu utajiri wa nchi yao lakini ni jambo la hatari

mno.Kama nikishindwa kulifanikisha lengo hilo, ninaomba pale utakapomaliza masomo yako uhakikishe unalikamilisha. Lazima uhakikishe unaendesha mapambano dhidi ya wezi a mali zetu.” Alisema Julius.Ambola alinesha kutomwelewa baba yake.

“Baba sijakulewa una maanisha nini? Kwani hii ramani umeitoa wapi? Aliuliza Ambola

“Sikiliza Ambola, ramani hii haikupaswa kuwepo hapa

kwani ni moja ya nyaraka za siri mno. Utakapokuwa mkubwa hakikisha ramani hii inafika kwa watanzania ili wafahamu kuhusiana na mali walizonazo. Najua kwa sasa hautaweza kunielewa lakini fanye kama nilivyokwambia" alisisitiza Julius.

"Baba mbona sikuelewi? aliuliza Ambola

"Kuna jambo lingine la mwisho ambalo ni muhimu sana" alisema Julius akamtazama mwanae.

“Endapo ikatokea bahati mbaya nikapatwa na jambo lolote baya au nikapoteza maisha, tafadhali kitu cha kwanza unachotakiwa kukifanya nenda katika ubalozi wa jamhuri ya kidemokrasia ya Congo mtafute mtu anaitwa Thomas Ngalula”

“Ni nani huyo Thomas Ngalula? Aliuliza Ambola.

“Ni mmoja wa wafanyakazi katika ubalozi huo.Ni rafiki yangu mkubwa.Usiende polisi au kwa mtu mwingine yeyote.Mtafute huyo mtu

niliyekwambia na utakuwa salama” alisema Julius.

“Kwa nini nikamuone yeye?

“Yeye ndiye atakayekusaidia kwa kila kitu. Hata funguo ya kuingilia katika nyumba hii ni yeye atakupatia” alisema Julius.

“Baba sijakuelewa kabisa kwa hayo unayoniambia.” Alisema Ambola.

“Yaweke akilini hayo niliyokwambia na uyatekeleze endapo nitapatwa na tatizo

lolote.” Alisema Julius. Macho ya Ambola yalianza kudondosha machozi.

“Pole sana Ambola. Najua niliyokuleza yanapita ufahamu wako lakini imenilazimu kukueleza kwani ndio ukweli wenyewe.” Alisema Julius.

“Baba uko kwenye hatari? Aliuliza Ambola

“Twende sasa tuondoke Ambola” alisema Julius. Walitoka ndani ya kile chumba wakaingia garini wakaondoka. Ilikuwa ni safari ya kimya kimya. Kichwa cha Ambola

kilijaa mawazo. Mambo aliyoambiwa na baba yake yalikuwa mazito na yalimchanganya.

****

Siku iliyofuata alifika dereva asubuhi akamchukua Ambola kumpeleka shuleni. Bado kichwa chake kilikuwa na mawazo kuhusiana na yale aliyoelezwa na baba yake siku iliyopita.

“Kwa nini baba aliamua kunieleza mambo yale? Nini alikimaanisha? Alijiuliza

Ambola akiwa njiani kuelekea shuleni.

Saa tano na dakika tisa, alifika mwalimu wa darasa na kumtaka Ambola kuchukua begi lake kwani anatakiwa kuondoka. Ambola alishangaa sana kwa udharura ule kwani muda wa kurejea nyumbani haukuwa umewadia.

“Mwalimu mbona muda bado? Kuna nini? Aliuliza Ambola.

“Baba yako anakuhitaji. Kuna dharura imetokea” alijibu mwalimu huku

akimsindikiza Ambola hadi katika maegesho ya magari. Jamaa mmoja aliyevalia suti nzuri nyeusi alikuwa amesimama nje ya gari la baba yake Ambola. Alipomuona Ambola alimsogelea akampokea begi.

“Wewe ni nani? Aliuliza Ambola kwa wasi wasi.

“Huyu ndiye aliyetumwa na baba yako kuja kukuchuka. ” Alisema mwalimu aliyekuwa ameongozana na Ambola.

“Simfahamu, sijawai kumuona. Unaitwa nani? Aliuliza Ambola

“Naitwa Lazaro, ni dereva wa baba yako” alijibu yule jamaa

“Dereva wa baba? Mbona baba anaendesha gari lake mwenyewe? Aliuliza Ambola

“Mimi ni dereva wake. Unadhani ningepataje funguo za gari lake kama si dereva wake? Aliuliza Lazaro huku akimfungulia Ambola mlango. Alimshukuru mwalimu akawasha gari wakaonodka.

“Baba yuko wapi? Kwa nini amekutuma wewe uje unichukue badala ya anko Samweli dereva wangu wa siku zote? Ambola aliuliza.

“Amenituma nikupeleke sehemu Fulani ambako anakusubiri. ” Alisema Lazaro halafu akaongeza sauti ya muziki akiashiria hakuhitaji maongezi zaidi.

Safari iliendelea kimya kimya hadi walipofika katika jumba moja kubwa. Geti lilifunguliwa gari likaingia ndani.

“Shuka tumefika. Baba yako ameelekeza uletwe hapa” alisema Lazaro.

Ambola alishuka garini, Lazaro akamuongoza wakaingia ndani ya ile nyumba. Kulikuwa na ukimya mkubwa. Sebuleni kulikuwa na wanawake wawili. Wote walikuwa wamevaa miwani myeusi kufunika macho yao huku wakivaa suruali za jeans zilizobana miili yao.

“Karibu Ambola. Twende huku” alisema mmoja wa wale wanawake. Ambola aliingiwa

na wasiwasi mwingi kwa hali aliyoikuta mle ndani. Mwanamke mmoja alitangulia, Ambola akafuata. Mlango wa chumba kimoja ulifunguliwa, Ambola akasukumwa ndani.

“Kaa pale kwenye kiti ! alifoka mwanamke mmoja. Ndani ya kile chumba kulikuwa na meza moja iliyokuwa na viti viwili. Juu ya ile meza kulikuwa na kamera. Ambola alitetemeka mwili.

“Baba yangu yuko wapi? Aliuliza Ambola. Tayari alikwisha hisi hatari.

“Kaa pale binti. Usitake nitumie nguvu !

“Kwani ninyi ni akina nani? Baba yangu yuko wapi? Aliuliza Ambola akiwa bado amesimama. Mwanamke yule alimsogelea akamnasa kofi zito Ambola akaanguka chini.

“Haraka inuka nenda kakae pale. ! Alifoka yule mwanamke. Ambola aliinuka pale chini akaenda kuketi katika kiti alichoelekezwa. Macho yake yalijaa machozi.

“Sikiliza Ambola. Kuna maswali nitakuuliza ninaomba

useme ukweli. Unanielewa? aliuliza yule mwanamke.

“Ndiyo” alijibu Ambola kwa hofu.

“Futa machozi haraka ! alisema yule mwanamke. Ambola alifuta machozi. Yule mwanamke aliwasha kamera halafu akauliza.

“Baba yako ana nyumba ngapi? Aliuliza yule mwanamke. Swali lile lilimshitua Ambola.

“Kwa nini ananiuliza kuhusu nyumba alizo nazo

baba? Nakumbuka ile nyumba aliyonipeleka jana baba alisema ni nyumba ya siri. Hakuna anayeifahamu. Hawa jamaa wanataka kuifahamu nyumba ile? Alijiuliza Ambola na mara meza ikagongwa.

“Jibu haraka ! alifoka yule mwanamke.

“Baba ana nyumba moja tu ambayo tunaishi” alijibu Ambola huku akitetemeka.

“Kwa nini unanidanganya Ambola? Aliuliza yule mwanamke

“Sikudanganyi dada. Baba ana nyumba moja tu ambayo tunaishi. Sifahamu kama ana nyumba nyingine.”

“Ambola unampenda baba yako? Aliuliza yule mwanamke

“Ndiyo ninampenda”

“Kama unampenda kwa nini unanidanganya?

“Ninakwambia ukweli dada naoma unielewe” alijibu Ambola.

“Kama hana nyumba nyingine unafahamu mahali anakoficha vitu vyake?

Amewahi kukuonesha? Aliuliza yule mwanamke.

“Hapana sifahamu na hajawahi kunionesha” alijibu Ambola kwa ujasiri huku macho yake yakiwa yamejaa machozi.

“Jana baba yako alikufuata shuleni akakuchukua. Mlikwenda wapi? Aliuliza yule mwanamke.

“Tulikwenda madukani. Alikwenda kuninunulia vitu mbali mbali”

“Baada ya hapo mlikwenda wapi?

“Tulirudi nyumbani. ” Alijibu Ambola. Yule mwanamke alisimama akatoka nje ya kile chumba. Baada ya dakika chache alirejea akamshika Ambola mkono akamchoma na kitu chenye ncha kali kama sindano. Ambola alipiga kelele kwa maumivu makali aliyoyapata.

“Sema ukweli. Jana mlikwenda wapi na baba yako? Aliuliza yule mwanamke

“Hatukwenda mahali ! alijibu Ambola huku akilia.

“Ambola nitakuchoma tena. Naomba unieleze ukweli.!

“Ninakwambia ukweli dada. Baada ya kutoka madukani tulirudi nyumbani.”

Yule mwanamke alimshika Ambola akamchoma tena na kile kifaa chenye ncha kali. Ambola alipiga kelele kubwa.

“Eleza ukweli” alisema yule mwanamke. Bado Ambola aliendelea kushikilia msimamo

wake wa kutokusema mahali alikopelekwa na baba yake. Mwanamke yule alimuachia Ambola akamtazama kwa jicho kali. Mlango ulifunguliwa akaingia mwanamke mwingine akamnong'oneza mwenzake kitu halafu akampatia boksi dogo, akatoka. Yule mwanamke alilifungua lile boksi dogo akampa Ambola pamba aweke mahali alipochomwa na kile kifaa chenye ncha kali palipokuwa panavuja damu.

“Sikiliza Ambola” alisema yule mwanamke.

“Tunahitaji makaratasi Fulani makubwa matatu. Umewahi kumuona nayo baba yako? Aliuliza yule mwanamke.

“Nahisi ni zile ramani alizonionesha baba jana akadai ni ramani za siri sana. Sasa nimejua kwa nini baba alinionya kuhusu kufahamu uwepo wa ramani zile. Hawa watu ni akina nani? Kwa nini baba alizichukua ramani zile? Alijiuliza Ambola.

“Ambola ninakuuliza umewahi kumuona baba yako na karatasi hizo? Aliuliza yule mwanamke.

“Hapana, sijawahi kumuona nazo. ” Alijibu Ambola.

“Una hakika? Aliuliza yule mwanamke.

“Nakwambia kweli dada sijawahi kumuona baba na hizo karatasi” alijibu Ambola. Yule mwanamke alimtazama kwa macho ya kikatili. Ambola aliogopa mno.

“Ambola unanidanganya. Tafadhali kama unafahamu mahali zilipo karatasi hizo niambie ili nikuache uende zako. Ukiendelea kunidanganya nitakukata masikio. ” Alisema yule mwanamke.

“Dada nakwambia ukweli. Sifahamu mahali ziliko hizo karatasi.” Alijibu Ambola. Yule mwanamke alifungua droo ya meza akatoa kisu kidogo kikali sana.

“Ninakukata masikio yako kwa sababu unanidanganya.

Niambie ukweli kabla sijakukata sikio! Alifoka.

“Dada unanionea bure. Sifahamu chochote kuhusu hizo karatasi” alisema Ambola

Hakuwa anatania. Yule mwanamke alimsogelea Ambola akamkamata vizuri kichwa chake akakata sehemu ndogo ya sikio. Aliacha baada ya Ambola kupiga kelele kubwa sana.

“Niambie wapi zipo karatasi? Aliuliza

“Sifahamu” alijibu Ambola huku akiruka ruka kwa maumivu makali.

Mwanamke yule alitoka ndani ya chumba akamuacha Ambola akilia. Aliingia katika chumba cha pili ambako watu watatu walikuwa wanafuatilia katika runinga mahojiano yale ya Ambola.

“Inaonekana huyu mtoto hafahamu chochote. Kama angefahamu zilipo karatasi zile angesema. Watoto hawawezi kuvumilia maumivu kiasi hiki” alisema yule mwanamke.

“Hata mimi ninakubaliana na Happy kuwa huyu mtoto hafahamu chochote.” alisema jamaa mwingine huku wote wakimtazama jamaa mmoja aliyekuwa amevaa suti ya bluu ambaye alionekana ndiye mwenye maamuzi ya mwisho.

“Sawa nakubaliana nanyi. Kama tumeshindwa kupata kitu kutoka kwa huyu mtoto, tusipoteze muda, tuingie katika plani nyingine. Julius akimuona mwanae hapa lazima atafunguka kila kitu.

Twendeni chumba D tafadhali” alisema yule jamaa.

Ambola alitolewa ndani ya kile chumba huku akilia kwani bado alihisi maumivu makali. Mlango wa chumba uliokuwa na alama D iliyoandikwa kwa rangi nyekundu ulifunguliwa Ambola akaingizwa ndani. Mwangaza ulikuwa hafifu sana. Kulikuwa na kidirisha kidogo kilichokuwa juu. Sakafuni alilala mtu ambaye alionekana kuumizwa sana. Taa iliwashwa halafu mtu yule

aliinuliwa na kuegemezwa ukutani. Hakuwa na nguvu.

“Julius ! Julius ! alisema jamaa mmoja aliyekuwa amevaa fulana iliyokatwa mikono huku akimtikisa yule mtu pale chini.

“Baba ! alisema Ambola kwa mshtuko baada ya kumuona baba yake.

Julius aliisikia sauti ya Ambola akapata nguvu akafumbua jicho moja la kulia. Jicho la kushoto halikuweza kufunguka. Lilikuwa limefumba. Damu iliganda

usoni ikionesha alikuwa amepigwa sana.

“Amb…. ! Julius alitaka kusema kitu akashindwa.

“Jamani muacheni baba yangu! Alipiga kelele Ambola huku akiruka ruka. Alikamatwa vyema akazibwa mdomo.

“Julius tumemleta mwanao Ambola. Huyu ni mwanao wa pekee na atauawa kama hautatupa kile tunachokitaka. Tuoneshe tafadhali mahali zilipo ramani zetu tukuache wewe na

mwanao” alisema yule jamaa mwenye suti ya bluu.

Julius alitaka kumtemea mate yule jamaa lakini kwa kuwa hakuwa na nguvu yaliishia kuchuruzikia kidevuni.

“Ambola tuambie tafadhali wapi zilipo zile karatasi tatu? Hii ni nafasi ya mwisho ya kumuokoa baba yako. Tunajua unafahamu mahali zilipo. Kama ukishindwa kutuonesha baba yako atauawa. Unataka ubaki yatima? Aliuliza yule jamaa. Ambola alimtazama

baba yake ambaye alikuwa katika maumivu makali na alijaribu kutaka kusema kitu lakini hakuweza. Hakuwa na meno mdomoni. Aling'olewa yote.

"Ramani zile lazima zina umuhimu mkubwa sana ndiyo maana baba hajaonesha mahali zilipo pamoja na mateso haya makali aliyoteswa. Alifahamu jambo hili lingeweza kumtokea ndiyo maana alinipeleka katika ile nyumba akiniandaa kwa tukio kama hili. Bado nayakumbuka

maneno yake.” Aliwaza Ambola halafu akazungusha macho mle chumbani akawatazama watu wote.

“Hii mijitu yote ni mikatili. Hata kama wakioneshwa mahali zilipo karatasi hawatatuacha hai. Hapa natakiwa kufanya chaguo moja. Aidha kumuokoa baba au kuziokoa ramani zile” aliwaza akamtazama tena baba yake.

“Sina uwezo wa kumuokoa baba kutoka katika mikono ya haya makatili. Inaniuma sana

lakini lazima nifanye uchaguzi. Nitaziokoa zile ramani. Baba alinisisitiza kwa namna yoyote ile lazima nihakikishe ninazilinda zile ramani. Lazima zina umuhimu mkubwa mno.” Aliwaza Ambola na kushtuliwa na sauti kali.

“Ambola tunataka jibu. Una sekunde tano tu za kufanya maamuzi au tutamuua baba yako. ” Alisema yule jamaa mwenye suti ya bluu halafu akatoa bastola. Ambola alitetemka sana.

“Tano ! alianza kuhesabu yule jamaa.

“Ambola uko tayari baba yako auawe? Tuoneshe tafadhali zilipo karatasi tuwaachie huru” alisema Happy mwanamke aliyekuwa anamtesa Ambola.

“Jamani naombeni msimuue baba yangu. Nitawaonesha mahali zilipo karatasi hizo. Ninafahamu zilipo” alisema Ambola.

“Good girl. ziko wapi hizo karatasi? Aliuliza yule jamaa mwenye suti ya bluu.

“Ziko chumbani kwake.”

“Sehemu gani chumbani kwake?

“Zipo katika kasiki anakoficha vitu vyake vya siri. Ni mimi pekee ninayeweza kulifungua.”

“Twende haraka sana utupeleke ukatuoneshe.”

“Mfungueni kwanza baba yangu” alisema Ambola

“Baba yako tutamuachia baada ya kuzipata karatasi hizo. Niamini tafadhali, ukitupatia karatasi

tutamuacha baba yako” alisema yule jamaa.

“Sawa twendeni niwapeleke” alisema Ambola halafu akamtazama baba yake huku akimuaga kimya kimya.

“Kwa heri baba. Tutakutana katika maisha mengine” alisema Ambola macho yake yakiwa yamejaa machozi.

Alitolewa mle ndani akaingizwa garini safari ya kuelekea nyumbani kwao ikaanza.

****

Gari mbili ziliwasili nyumbani kwa akina Ambola. Mtumishi wa ndani alifungua geti gari zile zikaingia ndani. Alishangaa sana kumuona Ambola akiwa amechafuka damu.

Moja kwa moja Ambola alichukua ufunguo wa akiba akafungua kitasa cha mlango wa chumba cha baba yake.

“Nataka aingie chumbani mtu mmoja. Wengine mtasubiri nje! Alisema Ambola kwa kujiamini.

“Wewe binti tafadhali usitufanyie mzaha. Tuoneshe haraka sana zilipo karatasi hizo” alifoka mmoja wa wale jamaa.

“Ni mimi ninayefahamu mahali zilipo karatasi hivyo mtafuata masharti yangu kama ninyi mlivyotoa sharti kuwa hamtamuachia baba yangu hadi pale mtakapozipata karatasi. Kama hamtaki kukubaliana nami niueni halafu tuone kama mtazipata hizo karatasi” alisema Ambola. Wote walishangazwa na ujasiri

mkubwa aliokuwa nao Ambola.

“Subirini nje” aliamuru yule jamaa mwenye suti ya bluu. Wale jamaa walipotoka Ambola aliufunga mlango halafu akaenda katika moja ya droo za kabati lililokuwa karibu na kitanda. Aliifungua huku yule jamaa akimtazama kwa makini mno.

“Ziko wapi hizo karatasi? Aliuliza.

“Ninatafuta funguo ya mahali zilipo.Naomba msaada tusogeze hili kabati” alisema

Ambola. Wakati jamaa akimsogelea, Ambola aligeuka haraka akiwa amelishika kopo la dawa ya kuulia wadudu akampulizia yule jamaa usoni.

“Aaaaghh ! alisema yule jamaa na kuweka viganja vya mikono katika macho yake.Ambola aliuchukua mkasi kwa kasi kubwa akamfuata yule jamaa na kwa kutumia nguvu zote alizokuwa nazo alimchoma nao sehemu za siri. Jamaa alipiga magoti huku akigugumia kwa maumivu makali. Hiyo ni fursa

aliyoihitaji Ambola. Haraka haraka alichukua kitanza mbali katika droo akakielekeza sehemu ukutani ambako kulikuwa na kioo fulani cheusi. Alibonyeza namba kadhaa halafu sehemu ya ukuta ikajiachia kukatokea uwazi. Alipanda kitandani haraka haraka akarukia ndani ya chumba kile kilichoonekana baada ya ukuta kuacha njia. Alibonyeza haraka haraka namba kadhaa zilizokuwa pembeni ya ule mlango na sehemu ile iliyojifugua ikajifunga. Hakupoteza muda

alienda katika kasha Fulani lililokuwa ukuitani akalifungua na kubonyeza kitufe chekundu. Mlio mkubwa ulianza kutoka katika kipaza sauti kilichofungwa nje ya nyumba ile.

Mlio ule uliwashtua sana wale jamaa waliokuwa nje ya chumba. Moja wao alijaribu kukiminya kitasa lakini mlango ulikuwa umefungwa kwa ndani.

“Deus ! Deus ! aliita yule jamaa lakini mkuu wao aliyekuwa ndani ya chumba

akigugumia kwa maumivu makali baada ya kuchomwa na mkasi mkali sana sehemu za siri bado alikuwa amekaa chini.

“Deus ! alita tena huku akigonga mlango. Deus alisikia sauti ile ikimuita. Alijiinua pale chini huku suruali yake ikiwa imeloa damu.Alienda mlangoni akaufungua. Wenzake walishangaa kumuona mkuu wao akiwa katika hali ile.

“Nini kimetokea ? Binti yuko wapi? Aliuliza Bonifasi.

“Aaagghh ! aagghh ! Deus alilalama kwa maumivu. Wenzake walimlaza chini.

“Deus nini kimetokea. Msichana yuko wapi?

“Find her ! Mtafuteni haraka ! alisema Deus.

Ndani ya chumba Ambola hakuonekana.Milango ya choo ilifunguliwa haraka lakini Ambola hakuonekana. Walichuguza dirisha lakini hakuna sehemu palipoharibiwa na kwa namna lilivyosukwa si rahisi kwa mtu kupenya.

“Deus haya mbona maajabu? Ambola yuko wapi?

Deus aliwaeleza kile kilichotokea mle ndani.

“Hukumuona mahali alikoelekea wakati mlikuwa wawili ndani?”

“Sikutegemea kabisa kama angeweza kunipulizia ile dawa kali.Wakati nikiwa nimeyafumba macho yangu kwa ukali wa ile dawa alinichoma na mkasi na sikumuona tena.” Alisema Deus.

“Haya ni maajabu makubwa sana.Huyu mtoto ana dawa? Anawezaje akatoweka tusimuone alikopita?” aliuliza Happy

“Ametokaje humu ndani? Amegeuka upepo akatoweka?

“Jamani msichana huyo yuko humu humu ndani. Find…. . ” Alinyamaza Deus baada ya kusikia hatua za watu wakija kwa kasi. Wote isipokuwa Deus walitoka mle chumbani wakakutana na walinzi kutoka kampuni ya ulinzi ambayo inalinda

nyumba ile. Gari lao halikuwa mbali na nyumba ile ya akina Ambola. Mara tu alipobonyeza kile kitufe cha kijani walipokea taarifa kuwa kuna hatari katika nyumba ile hivyo walifika haraka sana.

“Ninyi ni akina nani? Aliuliza mmoja wa wale walinzi.

“Ninyi ni akina nani? Aliuliza Bonifasi.

“Sisi ni walinzi kutoka kampuni ya ulinzi ya Chemi Chemi. Sisi ndio tunaolinda nyumba hiii. Tumepokea

taarifa kuna hatari hapa. Nini kinaendelea hapa? Aliuliza mzee mmoja kutoka kampuni ile ya ulinzi.

“Mzee tafadhali wakusanye vijana wako muondoke humu ndani haraka sana. Msiingilie mambo yasiyowahusu” alisema yule jamaa.

“Sisi ni walinzi wa hii nyumba. Tunahitaji kujua ninyi ni akina nani? Mnafanya nini hapa? Aliuliza kwa ukali kiongozi wa walinzi wale. Mmoja wa wale jamaa

alipandisha juu koti lake ikaonekana bastola.

“Naomba mtoke nje haraka sana kabla sijawamaliza nyote” alisema yule jamaa kwa ukali.

Walinzi wale waliingiwa na baridi. Hawakuwa na silaha ilhali wenzao walikuwa na silaha za moto. Walibaki wamesimama wakiwa wameduwaa hawajui la kufanya.

“Tokeni nje ! alifoka yule Bonifasi.

Walinzi wale walitoka nje, kiongozi wao akachukua simu akaanza kuwasiliana na ofisi yao kuu kuomba msaada.

“Deus tuondoke. Mambo yameharibika hapa”

“Hatuwezi kuondoka bila ramani” alisema Deus

“Deus tuondoke. Mambo yameharibika. Hawa mgambo wameshaharibu kila kitu. Tutarejea tena wakati mwingine kwa sababu tumeshajua kuwa ramani zipo humu ndani”

“Sawa tuondoke” alisema Deus. Walimsaidia kusimama. Huku akichechemea alitoka ndani ya chumba.

“Msichana mshenzi yule ameniumiza sana” alisema Deus

“Tutampata tu usihofu. Tutarudi tena” alisema jamaa mwingine. Waliingia katika gari lao wakaondoka wakiwaacha wale walinzi wa kampuni binafsi wamesimama wakiwakodolea macho.

Yote yaliyokuwa yanaendelea, Ambola aliyaona

kupitia runinga ndogo iliyounganishwa na kamera zote zilizofungwa katika ile nyumba. Aliwashuhudia wale jamaa wakiingia garini wakaondoka.

“Namshukuru sana baba kwa kunionesha uwepo wa chumba hiki ambacho alikiandaa endapo kutatokea hatari. Kama si hivyo huenda na mimi hivi sasa ningekwisha uawa. Wale watu ni makatili mno. ” Aliwaza Ambola akiwa bado ndani ya kile chumba.

“Kwa sasa sitakiwi kuendelea kukaa hapa. Natakiwa kuondoka. Natakiwa niende katika u balozi wa jamhuri ya kidemokrasia ya Congo nikaonane na Thomas Ngalula kama baba alivyonielekeza. ” Aliwaza Ambola akatoka ndani ya kile chumba akawafuata wale walinzi ambao bado walikuwa wamesimama wakijadiliana. Aliwasalimu na kuwashukuru kwa kufika kwa haraka.

“Wale watu ni akina nani? Aliuliza kiongozi wa walinzi wale.

“Ni majambazi . Walinifuata shuleni wakanileta hapa niwaoneshe mahali baba anakoficha pesa zake. Nilifanikiwa kuwadanganya nikabonyeza kile kitufe kilichowapa ninyi taarifa. Ahsanteni sana” alisema Ambola

. “Wale watu kweli ni majambazi. Hata sura zao zinaonesha ukatili mkubwa sana. Baba yako mbona simu

yake haipatikani? Aliuliza kiongozi wa walinzi wale.

“Sifahamu kwa nini” alijibu Ambola halafu akaelekea chumbani kwake akakusanya nguo na vitu vyake muhimu akaviweka katika sanduku dogo. Wakati akipakia vitu vyake mtumishi wao wa ndani aliingia mle chumbani na kushituka.

“Unasafiri? Aliuliza

“Wale jamaa wameniogopesha sana. Ninakwenda kukaa kwa rafiki yangu kwa muda. Nitarejea

baada ya wiki 2” alijibu Ambola.

“Baba anafahamu? Aliuliza Filomena

“Nitamjulisha. Wale watu nusura waniue leo” alisema Ambola

“Ambola nimeogopa sana. Wale jamaa hawatarudi tena?”

“Usiogope dada Filomena. Ulinzi upo. Hawawezi kurudi tena”

“Walinzi wenyewe hawa? Filomena alionesha wasiwasi.

“Dada mimi naondoka. Nitarejea baada ya wiki mbili” alisema Ambola na kulikokota sanduku lake dogo akatoka.

****

Teksi aliyopanda Ambola ilimfikisha katika geti la ubalozi wa jamhuri ya kidemokrasia ya Congo. Alishuka, akamlipa dereva hela yake halafu akaelekea katika chumba cha walinzi. Aliwasalimu, wakamuuliza shida yake akawaeleza anamtafuta Thomas Ngalula.

Mlinzi mmoja alichukua simu akapiga mapokezi akazungmza na mtu wa mapokezi halafu akamuelekeza Ambola sehemu ya kwenda. Ambola alilikokota sanduku lake akaenda hadi mapokezi ambako alijiandikisha kama mgeni wa Thomas Ngalula. Alielekezwa aketi sofani. Baada ya dakika kumi alitokea jamaa mmoja mnene akamfuata Ambola.

“Hujambo ? Aliuliza yule jamaa.

“Sijambo. Shikamoo”

“Marahaba. Mizigo yako iko wapi?

“Ni hili sanduku moja” alijibu Ambola

Yule jamaa alilibeba sanduku lile akamtaka Ambola amfuate. Waliingia katika gari yenye rangi nyeusi wakaondoka.

“Wewe ndiye Thomas Ngalula? Aliuliza Ambola wakiwa garini.

“Hapana si mimi ila ninakupeleka kwake” alijibu yule jamaa. Ambola

hakumuuliza tena swali lingine. Safari iliendelea hadi walipofika katika nyumba moja yenye bati la kijani iliyoko eneo tulivu la Sinzwe. Mara tu gari liliposimama mwanamke mmoja alitoka ndani na kulipokea sanduku la Ambola akawakaribisha ndani. Zilipita dakika chache akatokea jamaa mmoja mwembamba mrefu. Alionekana alitoka kulala.

“Karibuni” alisema

“Ahsante sana. Mkuu nimekuletea mgeni wako”

“Karibu sana Ambola.” Alisema yule jamaa ambaye Ambola alimuona kwa mara ya kwanza.

“Ahsante shikamoo” alisema Ambola.

“Marahaba” alisema yule jamaa ambaye moja kwa koja Ambola alijua ndiye Thomas Ngalula.

Thomas alimgeukia yule jamaa mnene akamshukuru kwa kufikishia mgeni wake, wakaagana akaondoka zake.

“Ambola karibu sana. Nimefurahi kukuona” alisema Thomas

“Wewe ndiye Thomas Ngalula? Ambola aliuliza.

“Ndiyo ni mimi”

“Nimekuja kukuona. Baba alinipa maelekezo nije nikuone wewe endapo atapatwa na matatizo” alisema Ambola na kumueleza Thomas kile kilichomtokea baba yake. Thomas aliinamisha kichwa chini kwa dakika kadhaa.

“Nimeumizwa sana. Julius ni rafiki yangu mkubwa.”

“Unawafahamu watu wale waliomteka baba? Aliuliza Ambola.

“Siwafahamu ila lazima ni watu hatari mno.” Alijibu Thomas

“Unawafahamu?

“Hapana siwafahamu” alijibu Thomas

“Kwa nini tusitoe taarifa polisi ili watafutwe? Nahitaji kujua hatima ya baba yangu. Nilimuacha akiwa katika hali

mbaya sana.Ameteswa mno.” alisema Ambola.

“Ambola hatuwezi kufanya hivyo.Utakuwa unajiweka wewe mwenyewe katika hatari kubwa.” Alisema Thomas

“Sasa tutafanya nini kumuokoa baba yangu? Aliuliza Ambola.Tayari macho yake yalijaa machozi.

“Kwa sasa hakuna tunachoweza kukifanya Ambola kumsaidia baba yako” alisema Thomas. Macho ya Ambola yalijaa machozi.

“Nafahamu ni jambo gumu lakini lazima nikueleze ukweli.Hakuna namna yoyote ambayo tunaweza kumsaidia baba yako kwa sasa. Alifahamu jambo hili litatokea ndiyo maana alifanya maandalizi mapema ili wewe uwe salama. Ninakusifu sana kwa akili uliyoitumia hadi ukaponyoka kutoka katika mikono yao. Wasingekuacha hai” alijibu Thomas.

“Namlaumu sana baba.Kwa nini alichukua ramani zao hadi amaingia

katika matatizo haya makubwa na wale watu? aliuliza Ambola.

“Hupaswi kumlaumu baba yako. Unapaswa kumpongeza. Baba yako ni shujaa. Kitu alichokifanya kina manufaa makubwa mno kwa nchi hii na kwa Afrika nzima.” Alisema Thomas.

Ambola aliinamisha kichwa akaanza kulia kwa kwikwi.

“Ambola usilie tafadhali.Jipe moyo japo unapitia kipindi kigumu sana” alisema Thomas.

“Thomas nini itakuwa hatima yangu? Nitakwenda wapi ambako nitajificha wa wale jamaa?” aliuliza Ambola.

“Utakaa hapa kwangu kwa siku chache wakati ninafanya mipango ya kukutafutia sehemu salama zaidi ambako utaishi. Usiwe na hofu nitahakikisha unakuwa salama muda wote. Hiyo ni ahadi niliyompa Julius.” Alisema Thomas. KIlipita kimya kifupi Ambola akauliza.

“Kwani baba anafanya kazi gani? Ramani zile amezitoa wapi? aliuliza Ambola.

“Ambola kuna mambo ambayo kwa umri wako hupaswi kuyafahamu. Kitu pekee kwa sasa ni kuhakikisha unakuwa sehemu salama na unamaliza masomo yako.Hicho ndicho alichokihitaji baba yako” alijibu Thomas.

“Thomas ninahitaji kufahamu kila kitu kuhusu baba yangu. Kama unafahamu

naomba unieleze tafadhali” alisisitiza Ambola.

“Ambola kwa sasa sintakueleza chochote ila kuna kitu kimoja tu ambacho unapaswa ukifahamu. Baba yako kuamua kukushirikisha katika siri hii kubwa hadi kukuweka katika hatari hii kubwa licha ya umri wako mdogo, ni kwa sababu maalum. Anakuandaa kwa ajili ya ukombozi wa rasilimali za nchi hii na Afrika kwa ujumla ambazo zinachotwa bila huruma na mabeberu. Mimi

ninatokea nchini Congo. Ni nchi tajiri kwa rasilimali lakini asilimia kubwa ya raia wake ni masikini sana. Zamani tulizoea kuona wezi wa rasilimali zetu ni watu wa kutoka mataifa ya mbali lakini siku hizi rasilimali zetu zinatafunwa hata na sisi wenyewe waafrika. Wapo watu wetu ambao wanashirikiana na mabeberu kupora utajiri wetu. Haya yote ni mambo ambayo baba yako amekuandaa uje uyashughulikie pindi utakapokuwa mkubwa. ” Alisema Thomas.

“Alinieleza jana lakini nitawezaje kupambana na watu makatili kama wale? Sina uwezo huo” alisema Ambola.

“Ambola hupaswi kukata tamaa. Hawa watu wamekatili uhai wa baba yako. Wanapaswa kuadhibiwa vikali. Kuanzia sasa fahamu umebeba jukumu zito. Unapaswa usome kwa bidii ili siku moja uje ufanye kile ambacho baba yako alikuelekeza ukifanye.” Alisisitiza Thomas.

Aliinuka akaenda chumbani kwake akarejea na mkebe mdogo.

“Baba yako alinipa mkebe huu ili siku ukija kwangu nikukabidhi. Ndani ya huu mkebe kuna funguo ya kufungulia ile nyumba zilimo ramani.Hakuna anayeweza kuingia mahali zilipo ramani bila kutumia funguo hii.” alisema Thomas. Ambola alielekezwa chumba atakacholala. Akiwa chumbani aliufungua mkebe ule akakuta

kuna msalaba na kijikaratasi kidogo kilichoandikwa.

“Msalaba huo ndio ufunguo wa kila kitu. Utunze zaidi ya mboni ya jicho lako”

Nyuma ya karatasi zile kuliandikwa namba kwa ajili ya kufungulia kasiki zilimo ramani.Ambola alikisoma kikaratasi kile kwa kukirudia. Aliuchukua msalaba ule akauvaa.

Siku tatu alizokaa nyumbani kwa Thomas zilikuwa ngumu. Hakuruhusiwa kutoka nje.

Alishinda chumbani akimlilia baba yake ambaye aliamini hatamuona tena.

Siku ya nne Thomas alirejea nyumbani mapema sana akamuita Ambola kwa ajili ya mazungumzo.

“Kuna chochote umekipata kuhusu baba yangu? Aliuliza Ambola.

“Mpaka sasa hakuna chochote nilichokipata kuhusu baba yako ila ninaendelea kufuatilia. Nikipata chochote nitakujuza.” Alijibu Thomas.

“Tafadhali naomba ufuatilie kujua hatima ya baba yangu kama wale jamaa walimuua au bado mzima” alisisitiza Ambola.

“Nitafanya hivyo” alisema Thomas halafu ukimya ukatawala.

“Ambola nimekuja kukujulisha kuwa mipango ya kukuondoa Dar es salaam imekamilika na utaondoka usiku wa leo.”

“Unanipeleka wapi? Aliuliza Ambola

“Utakwenda Kigoma”alijibu Thomas

“Kigoma? Aliuliza Ambola kwa mshangao.

“Ndiyo. Utakwenda Kasulu Kigoma. Utaishi katika kambi ya wakimbizi wanaotoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo. ”

“Mimi nikaishi katika kambi ya wakimbizi? Ambola alishituka sana.

“Ndiyo Ambola. Sehemu pekee ambako utakuwa salama

kwa sasa ni katika kambi ya wakimbizi.”

“Hapana sintaenda huko. Siwezi kuishi katika kambi ya wakimbizi. ! Alisema Ambola

“Ambola nisikilize vizuri. Baba yako alikuelekeza kwangu ili nikusaidie uwe salama. Mahali ninakotaka ukaishi kwa muda ndiko mahali pekee salama kwako kwa sasa. Watu wale waliomchukua baba yako ni mtandao mkubwa, wamesambaa karibu nchi nzima. Hakuna sehemu ya

kukimbilia. Ni watu wenye nguvu na uwezo. Mahali pekee ambako utakuwa salama ni katika kambi ya wakimbizi. Hakuna yeyote anayeweza akafikiri unaweza ukaishi mahali hapo. Tayari mipango yote imekamilika utasajiliwa kama mkimbizi kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo. Nitakupa maelekezo yatakayokusaidia ukiwa hapo kambini. Kitu kizuri ni kwamba unazungumza vizuri lugha yya Kifaransa hiyo itakusaidia sana kwani

wacongo wengi wanazungumza Kifaransa.”

Ambola alikosa neno la kusema. Haikuwahi kumuingia akilini kuwa siku moja angeishi kama mkimbizi.

“Ambola utapitia kipindi kigumu sana. Maisha ndani ya kambi si rahisi hata kidogo. Pamoja na ugumu wake lakini nakuomba uvumilie. Ninakuahidi sintakuacha peke yako. Mkuu wa kambi hiyo ni rafiki yangu hivyo nitakuwa nikifuattilia maendeleo yako.” Alisema Thomas

“Nitakaa kwa muda gani hapo kambini? Aliuliza Ambola

“Sifahamu utakaa kwa muda gani lakini wakati ukiwa hapo kambini nitaendelea na mipango mingine ya wapi uelekee. Yawezekana ukakaa kambini kwa mwezi mmoja, miezi au hata mwaka. Itategemea jinsi mipango niipangayo itakavyokamilika. Ambola nakusisitiza hata kama itachukua muda gani kwa wewe kuishi hapo kambini kamwe usikate tamaa.

Vumilia. Usithubutu kutaka kutoroka kwani utakuwa umejiweka katika hatari kubwa. Hiki ni kipindi kifupi cha kiza unakipitia lakini baada ya kiza huja nuru hivyo vumilia kizani ili uione nuru. Haya unayoyapitia si kwa faida yako bali ni kwa faida ya nchi yako na Afrika kwa ujumla” Alisema Thomas.

MIEZI MINNE BAADAYE

KASULU - KIGOMA

Haikuwa ni ndoto tena. Ambola aliyaanza maisha ya ukimbizi katika kambi ya wakimbizi wanaotoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo iliyopo Kasulu Kigoma. Hayakuwa maisha rahisi hata kidogo kwake. Kila jua lilipochwea alitamani lisichomoze siku inayofuata. Kila usiku alilia machozi mengi na wakati mwingine alimlaumu sana baba yake kwa kumuingiza katika maisha

yale. Aliyakumbuka maisha mazuri aliyokuwa akiishi jijini Dar es salaam. Miezi michache iliyopita alikuwa akiishi katika jumba kubwa, hakuelewa nini maana ya shida. Alikuwa na gari maalum la kumpeleka shule na kokote alikohitaji kwenda. Haikuwahi kumjia hata ndotoni kuwa simu moja angegeuka mkimbizi.

“Bado nitaendelea sana kumlaumu baba kwa kuniingiza katika maisha haya. Sikupaswa kuteseka namna hii” aliwaza Ambola.

“Thomas amekuwa anasisitiza eti nivumilie maisha haya. Nimechoka. Siwezi tena kuendelea kuishi hapa kambini. Tuna nyumba kubwa Dar es salaam na kila kitu kizuri. Siwezi kuendelea kuishi maisha haya ya kulala katika hema. Lazima niondoke mahali hapa. Lazima nitoroke nirejee Dar es salam. Kama wale jamaa watanifuata tena nitawapa ramani zao ili niishi kwa amani. Siwezi kuendelea kuteseka hapa kwa kitu ambacho sikielewi” aliwaza Ambola.

Ambola alishindwa kuendelea kuvumilia. Miezi minne ya kuishi katika kambi ile ilimtosha na hakuhitaji tena kuendelea kuishi mahali pale hivyo alikata shauri kuanza utafiti ni namna gani atakavyoweza kutoroka pale kambini kurejea Dar es salaam. Alianza mipango yake kwa kuyasoma mazingira ya kambi na jinsi gani anaweza akatoroka.

“Nikifanikiwa kutoka ndani ya kambi hii nitakwenda kujieleza katika kanisa lolote

au msikiti na kuomba msaada wa kurejeshwa Dar es salaam. Sijali kitakachotokea lakini sitaki kuendelea kuishi maisha haya" aliwaza Ambola.

Siku moja akiwa katika harakati za kupanga mpango wake wa kutoroka, aliitwa na mzee mmoja ambaye umri wake ulikaribia miaka sabini.

"Binti nimekuwa ninakufuatilia tangu ulipofika hapa. Nimegundua u tofauti kabisa na wasichana wengine wa umri wako walioko hapa kambini. Unaweza ukaniambia

unatokea sehemu gani ya Congo? Aliuliza yule mzee. Ambola alimpa maelezo yale aliyofundishwa na Thomas.

“Pamoja na maelezo yako lakini bado kuna kitu ninakiona kwako. Katika kukufuatilia sijawahi kukuona hata siku moja ukizungumza lugha ya asili ya Congo. Umekuwa ukitumia kifaransa na kiingereza pekee. Ni kwa nini hutaki kutumia lugha yako ya asili? Aliuliza mzee yule.

“Kwa kuwa nimeshaamua kuondoka mahali hapa ngoja nimueleze ukweli huyu mzee. Inaonekana tayari wameanza kunitilia mashaka.” Aliwaza Ambola

Alimueleza yule mzee kisa chote hadi yeye kujikuta yuko mahali pale. Mzee yule ambaye alijitambulisha anaitwa Alfred Ngalamulume aliangusha chozi. Aliumizwa mno na simulizi ile ya maisha ya Ambola.

“Pole sana binti. Hadithi ya maisha yako imenichoma

mno. Nimeumia kwa sababu kinachosababisha haya yote kutokea hadi sisi sote kujikuta mahali hapa ni mali ambazo Mwenyezi Mungu mtukufu ametuwekea katika ardhi yetu ya Afrika. Mali hizo ambazo tumepewa zitunufaishe sisi na vizazi vyetu tufurahie uwepo wetu hapa duniani zimegeuka laana na kutuamgamiza. Hii inaniumiza mno" alisema mzee Alfred ambaye mwenyewe alipenda kuitwa Fredo.

“Mimi hadi kufika umri huu nimezunguka karibu bara zima la Afrika. Ni bara tajiri sana. Mungu amelipa upendeleo mkubwa wa rasilimali. Kitaaluma mimi ni daktari bingwa wa figo. Kazi yangu hiyo imenifikisha katika nchi mbali mbali barani Afrika na hata nje ya Afrika. Nimeona mengi. Nimejifunza mengi lakini pamoja na usomi wangu leo niko hapa katika kambi ya wakimbizi. Inaniumiza mno. Kwa bahati mbaya sana umri umeenda. Nina miaka sabini na nne kwa sasa. Laiti

ningekuwa na uwezo wa kurejesha umri nyuma nikawa kijana tena ningefanya mambo makubwa sana kuhakikisha dhuluma hii tunayofanyiwa inakoma. Ningekuwa kijana tena nisingekubali kuona kuna kambi kama hizi za wakimbizi. Kwa mkono wangu ninaapa ningepambana na wanyonyaji hawa pamoja na vibaraka wao. Tumefikishwa hapa tulipo kwa sababu ya usaliti wa wenzetu wachache ambao wako tayari kuwa vibaraka wa mabeberu na kupata faida kidogo huku wakiwaacha ndugu zao

tukiteseka namna hii. Tumefika hapa tulipo kwa sababu ya uroho wa madaraka wa viongozi wetu tunao waweka madarakani ambao badala ya kusaidia kukwamua jamii za watu masikini wao wamekuwa wanajali matumbo yao na familia zao. Wameturudisha nyuma mno na kwa hili viongozi wetu wanalo la kujibu mbele za Mungu. ” Alinyamaza kwa muda akamtazama Ambola.

“Binti najua unateseka sana kwa sasa na hujui ni kwa

nini unateseka. Umeniambia unamlaumu baba yako kwa kukuingiza katika shida hizi. Mimi simlaumu hata kidogo kwani hajakutesa bali amekuingiza katika mafunzo. Ninamsifu sana baba yako. Ni shujaa. Amekubali kuteswa na yawezekana amepoteza uhai wake kwa ajili ya kupigania ramani hizo zinazoonesha utajiri wote ulipo hapa nchini na katika bara zima la Afrika. Kama amekufa basi amekufa kishujaa akiitetea nchi yake. Nakuomba uvumilie binti ili siku moja uje kufanya kile

ambacho baba yako amekusudia ukifanye. Kuanzia sasa anza kuisoma historia ya nchi yako na bara zima la Afrika. Unatakiwa ufahamu mahali nchi yako ilipotoka na ilipo sasa. Nchi hii imebarikiwa sana. Nimekwambia nimezunguka katika nchi zote za bara hili la Afrika lakini sijaona nchi ya kipekee kama hii ya Tanzania. Nchi hii inapaswa kulindwa kwa kila namna ili isitoke katika misingi yake imara iliyojengwa na waasisi wa taifa hili. Tungekimbilia wapi sisi

kama Tanzania isingekuwa na amani? Tunaiona nchi hii kama ile nchi ya ahadi. Ilindeni nchi yenu. Baba yako ameonesha mfano nawe unapaswa kufuata nyayo zake. ” Alinyamaza mzee Fredo. Ambola alikuwa kimya kabisa akimsikiliza.

“Ninafuatilia mwenendo wa Tanzania. Nimeanza kuingiwa na hofu. Kuna watu hawana nia njema na nchi hii. Kinachonisikitisha watu hao ni wazawa wa nchi hii. Watu kama hao si wa kuwaacha hata

kidogo wakatimiza malengo yao na kuibomoa hii nchi. Vijana kama ninyi mnapaswa mpambane na watu kama hao ambao hawaoni ugumu kuwaingiza hata katika machafuko ili mradi kufanikisha mipango yao na ya wale waliowatuma. Ninarudia tena kumsifu baba yako kwa alichokifanya. Nina uhakika mkubwa kwamba watu hao waliomteka ili awaoneshe mahali zilipo hizo ramani ni miongoni mwa hao ninaowasema kwamba wana ajenda zao binafsi kwa nchi hii.

Yawezekana haya ninayokwambia sasa usiyaelewe lakini siku moja utayakumbuka. Ninarudia kukusisitiza vumilia. Wewe ni wa muhimu sana. Soma historia. Ifahamu vyema nchi yako. Utakapofika wakati wa kuipigania watafute vijana wenzako wazalendo muunganishe nguvu na muhakikishe dhuluma na unyonyaji wa rasilimali zenu hauendelei tena. Kwa sasa nenda kapumzike. Nitakuwa ninazungumza nawe mara kwa mara kukupa moyo na

kuhakikisha malengo ya baba yako yanatimia” alisema mzee Fredo. Ambola alimuaga akaondoka zake.

Aliyatafakari maneno ya mzee Alfredo lakini hakuyaelewa. Bado aliendelea na mkakati wake wa kutoroka pale kambini. Hakutaka kuendelea kuteseka mahali pale.

Akiendelea na mipango yake ya kutoroka, Ambola alitembelewa na mgeni. Alitembelewa na Thomas Ngalula. Kitu cha kwanza

alichotaka kukifahamu baada ya kuonana naye ni kuhusiana na baba yake. Thomas alimjulisha kuwa hakuwahi kuwasiliana na Julius na wala hajui mahali alipo. Jibu lile lilimnyong'onyeza sana Ambola.

"Ambola najua ni jambo gumu lakini lazima tukubali kuwa baba yako hutamuona tena. Kwa sasa tujielekeze katika mipango inayofuata" alisema Thomas.

"Thomas naomba uniondoe mahali hapa. Sitaki

tena kuendelea kukaa hapa. Nimechoka na mateso haya" aliomba Ambola huku akilia.

"Ambola nilipokuleta mahali hapa nilikuomba uwe mvumilivu. Usiwe na haraka ya kuondoka mahali hapa. Kama una mipango ya kutoroka iache mara moja kwani utazidi kujiweka katika hatari kubwa."alisema Thomas.

"Sitaki tena kuendelea kuishi hapa. Tafadhali niondoe katika mateso haya. Ninataka nikaishi maisha yangu ya

kawaida hata kama ni hatari. ” aliomba Ambola.

“Ambola utaondoka hapa kwa mipango maalum lakini ukiondoka kiholela utahatarisha maisha yako na hutakuwa unamtendea haki baba yako. Mipango ya kukuondoa hapa inakwenda vizuri ndiyo maana nimekuja hapa kuzungumza nawe kukupa taarifa za kile kinachoendelea” Thomas alinyamaza kidogo. Ambola alionesha kuwa na kiu ya

kutaka kusikia kutoka kwa Thomas.

“Utaondoka hapa kambini hivi karibuni. ”

Kwa mara ya kwanza tangu amefika katika kambi ile, Ambola alitabasamu.

“Lini nitaondoka mahali hapa? Aliuliza Ambola

“Hivi karibuni kuna watu watakuja hapa kukuchukua”

“Kunichukua? Ambola alishangaa.

“Ndiyo watakuja watu Fulani kukuchukua.”

“Kunichukua kunipeleka wapi? Ni wale jamaa wanaotafuta ramani? Aliuliza Ambola

“Ambola kuna mambo ambayo lazima nikufahamishe uyafahamu. Ila naomba kile nitakachokwambia kibaki siri yako usimueleze mtu yeyote.” Alisema Thomas

“Hii ni kambi ya wakimbizi wa kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo. Hawa wote wako hapa kutokana na

machafuko yanayoendelea nchini mwao. Kwa nini machafuko hayaishi nchini mwao na kuwasababisha mateso makubwa watu hawa? Ni kwa sababu kuna watu wanaofaidika na machafuko hayo. Nchi yetu ni tajiri kama ilivyo nchi yenu lakini raia wake hawafaidiki na utajiri wake zaidi ya mateso kama haya. Watu hao wachache ambao wanaendesha machafuko nchini kwetu wanatumiwa na watu kutoka mataifa ya nje ambao ninyi hapa Tanzania mnawaita

mabeberu. Nisiende ndani sana yawezekana usinielewe.” Thomas alinyamaza kidogo.

“Kuna mipango ambayo si mizuri inafanywa na Mabeberu dhidi ya nchi kumi za Afrika zikiwamo jamhuri ya kidemokrasia ya Congo na Tanzania. Mipango hiyo inazilenga nchi zile zenye utajiri mkubwa wa rasilimali . Mipango hiyo ni kuhakikisha wanawaingiza watu wao katika nafasi za juu za uongozi wa nchi hizo kumi wanazozilenga. Mipango hii si ya muda mfupi.

Ni mipango ya muda mrefu. Japo itachukua muda mrefu kukamilika lakini hilo si tatizo kwao wanachokihitaji ni mipango yao kufanikiwa. Maandalizi ya mipango hiyo yamekwisha anza. Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo kwa sasa inaongozwa na Jenerali Salvatory Mamba. Huyu aliingia madarakani kufuatia mapinduzi ya kijeshi. Huyu anaongoza serikali ya kijeshi na haijulikani lini ataondoka madarakani. Rais huyu amekuwa mwiba mkali kwa mabeberu waliokuwa

wakinufaika na rasilimali za Congo. Ni kwa sababu hiyo kumekuwa kukiibuka vikundi vingi vya uasi kila wakati. Karibu vikundi hivi vyote vinafadhiliwa na mabeberu ili kuipinga serikali ya kijeshi ya Rais Mamba. Machafuko yameendelea na kupelekea idadi kubwa ya wakimbizi unaowaona hapa kambini. Pamoja na njia hiyo ya mabeberu ya kupandikiza makundi ya waasi, bado hawajafanikiwa. Jenerali Salvatory amezidi kuwa imara kutokana na kuwa na jeshi

imara. Inasemekana anaungwa mkono na nchi moja japo haijulikani ni nchi gani. Mabeberu wameamua kuja na mpango mwingine wa kuleta mabadiliko nchini Congo. Wameanza kutengeneza mtandao wa wacongo walio nje ya nchi yao ili kuwaandaa kwa mapinduzi. Ni mpango wa muda mrefu kama nilivyokwambia lakini utekelezaji wake tayari umeanza. Mtandao umekwisha anza kutengenezwa kimya kimya. Si kwa jamhuri ya kidemokrasia ya Congo pekee

bali pia kwa zile nchi kumi nilizokwambia. Kwa sasa wanatafutwa wasichana hamsini wa umri wako wenye asili ya Congo ili waanze kupewa mafunzo na kuwapandikiza chuki dhidi ya nchi yao. Ninataka kuitumia fursa hiyo kukuondoa hapa kambini" Alisema Thomas huku Ambola akiendelea kumshangaa.

"Mafunzo hayo mimi hayanihusu kwa sababu mimi ni mtanzania." Alisema Ambola.

“Hakuna atakayefahamu kama wewe ni mtanzania. Kila mtu atafahamu wewe unatokea Congo na umechukuliwa katika kambi ya wakimbizi. Taarifa zako zote zimekwisha tengenezwa. Nataka uitumie fursa hii usome na upate mafunzo ili kujiandaa kwa kazi ambayo baba yako alitaka uifanye. Utaishi katika familia ya watanzania lakini jitahidi hata siku moja usije ukatamka kuwa wewe ni mtanzania. Chunga maneno yako, chunga nyendo zako kwani hawa watu watakuwa wanakuchunguza

kwa siri bila wewe kujua hivyo hata siku moja usithubutu kumweleza mtu yeyote historia yako, usitembelee maeneo yale uliyokuwa ukiishi na wazazi wako. Waepuke kabisa marafiki zako wa zamani wanaokufahamu. Nafahamu ni mateso makubwa utayapitia lakini vumilia. Yabadili kabisa maisha yako.” Alisema Thomas na kunyamaza kidogo.

“Kwa nini baba hakuimaliza kazi yake hadi aniachie mzigo huu mimi? Aliuliza Ambola

“Alikuwa na nia hiyo lakini muda haukuruhusu.Hili si jambo jepesi hata kidogo. Ni jambo zito kwani linagusa maslahi ya watu wazito. Linagusa maslahi ya mabeberu hivyo linahitaji umakini sana. Ambola usiwe na hofu yoyote mimi nipo nitakusaidia kuhakikisha unalifanikisha jambo hili. Nilimuahidi hivyo Julius na nitahakikisha ahadi hiyo inatimia. Utaandaliwa kwa ajili ya misheni inayoitwa Congo mpya wakiamini wewe unatokea Congo. Wakati ukiendelea na misheni hiyo

wewe utakuwa na misheni ya siri ya kuwachunguza watu hao mipango yao dhidi ya Tanzania. Kwa pamoja tutatafuta namna ya kuharibu mipango yao isifanikiwe. Baada ya kuhakikisha mtandao huo umesambaratishwa ndipo watanzania watakapoufahamu ukweli kuhusiana na utajiri uliofichwa wasiufahamu. Usiwe na hofu utaelewa tu kadiri siku zinavyosonga.Mimi pia nipo katika mtandao huo nbitakuwa nawe karibu kukupa mwongozo nini cha kufanya" alisema Thomas.

Ambola alikubaliana na mpango ule wa Thomas. Baada ya wiki 2 Ambola alichukuliwa pamoja na msichana mwingine aliyeitwa Maria wakapelekwa jijini Dar es salaam kuanza maisha mapya huku Ambola akijitahidi kufuata maelekezo aliyopewa na Thomas kuhusu kuificha siri yake isijulikane.

****

Ambola alikurupuka na kulitupa shuka alilojifunika baada ya mkono wake wa kulia kupita shingoni bila kuugusa mkufu wake ambao haukuwahi kutoka shingoni mwake.

“Ambola kuna nini? Aliuliza mtu aliyekuwa pembeni yake.

“Mkufu wangu ! alisema Ambola huku akitoka kitandani na kuanza kuusaka mkufu katika nguo zake. Alionekana kuchanganyikiwa.

“Ambola mkufu wako uko chini ya mto. Hukumbuki uliuvua na kuuweka chini ya mto? Yule mtu aliyekuwa naye kitandani alimwambia.

“Niliuvua? Ambola alishangaa.

“Ndiyo. Uliuvua na kuuweka chini ya mto.” Alisema mzee yule. Haraka haraka Ambola aliuinua mto na kuukuta mkufu wake.Alitabasamu.

“Thank you Lord. ” Alisema Ambola huku akishusha pumzi. Hakupoteza

muda akauvaa mkufu ule aliouthamini sana.

“Nusura roho yangu initoke baada ya kuukosa mkufu wangu. Nashangaa ilikuaje hadi nikautoa mkufu huu ambao haujawahi kutoka shingoni mwangu. Nimefanya kitu cha kijinga sana” aliwaza Ambola.

“Mbona umeshituka namna hiyo baada ya kuukosa mkufu? aliuliza mzee yule ambaye alikuwa amekaa kitandani akimtazama Ambola.

“Mkufu huu hautakiwi kutoka shingoni mwangu ndiyo maana nilishituka nilipoukosa.” alijibu Ambola akasimama na kutembea kwa mwendo wa maringo kuelekea maliwato. Mzee yule alimtazama Ambola kwa macho yaliyojaa matamanio. Alipotoka maliwato alirejea kitandani.

“Ambola wewe ni mzuri sana. Nikuonapo ukitembea hasa ukiwa mtupu ninahisi mwili wangu wote unanitetemeka.”

Ambola alitabasamu baada ya kuambiwa maneno yale.

“Ahsante ninashukuru kwa sifa hizo.” Alisema Ambola

“Sipati picha mama yko mzazi alikuwa mrembo kiasi gani” alisema mzee yule.

“Tafadhali naomba usinikumbushe kuhusu wazazi wangu.” Alisema Ambola

“Samahani.”alijibu yule mzee. Naye aliinuka akaingia maliwato na alipotoka alirejea tena kitandani.

“Mzee Perfect nina swali nataka kukuuliza” alisema Ambola

“Ambola nikwambie mara ngapi tunapokuwa faragha sitaki unite mzee? Aliuliza huku akimtazama Ambola.

“Nataka unite jina langu Perfect. Kwa nini unataka kunizeesha haraka hivyo? Aliuliza mzee Perfect ambaye kichwa chake kilijaa mvi. Ambola alitabasamu na kusema.

“Nisamehe kwa kusahau darling. Ninachohitaji kujua ni

vipi siku moja mama Bernadetha akigundua mimi nawe tuna mahusiano? Aliuliza Ambola.

“Hawezi kugundua” alijibu Perfect kwa kujiamini.

“Mama Bernadetha ana mtandao mkubwa anaweza akafahamu” alisema Ambola.

“Hata kama akifahamu hakuna tatizo. Mimi nawe hatuna mahusiano yoyote ya kibaolojia. ”alisema mzee Perfect huku akimfanyia ishara Ambola amuwekee kinywaji katika glasi.

“Japokuwa hatuna mahusiano ya kibaolojia lakini ninakuchukulia kama baba yangu. Wewe ndiye uliyenilea kama mwanao nilipotolewa kambini Kigoma” alisema Ambola. Perfect alikunywa funda la kinywaji, akatabasamu na kusema.

“Lakini ni wewe uliyeniwekea mitego hadi nikanasa. Umenionjesha asali tamu na siwezi kuiacha tena.Umenirejeshea ujana” Alisema Perfect. Ambola alitazama chini. Alihisi aibu.

“Ambola kwa nini uliamua kunitega hadi nikanasa na kuwa mjinga kwako? Kwa sasa sisikii la mtu juu yako.Ninatamani hata nikufanye mke wa pili” alisema mzee Perfect na kumfanya Ambola atoe kicheko kikubwa.

“Nilikuwa nayafanyia majaribio mafunzo niliyopewa namna ya kumshawishi mwanaume yeyote yule aanguke kwangu.” Alisema Ambola.

“Kwa hilo umefaulu Ambola.Kama umeweza

kuninasa mimi na hata kile chuma Gosu Gosu , hakuna mwanaume anayeweza akaponyoka katika mtego wako. Utatusaidia sana katika kutafuta taarifa mbali mbali kutoka kwa watu tunaowahitaji kwani mambo yameanza kupamba moto” Alisema mzee Perfect.

“Mzee…oh samahani Perfect nataka kujua maendeleo ya Gosu Gosu” alisema Ambola

“Kwa sasa muondoe Gosu Gosu kichwani mwako.

Umekwisha maliza kazi yako uliyotumwa kwake hana umuhimu tena kwako.Tayari tumekipata kile tulichokuwa tunakihitaji kwake” alisema mzee Perfect.

“Ninataka tu kufahamu kama yuko salama. Alinipenda mno yule jamaa na alikuwa tayari hata kufunga ndoa nami muda wowote lakini nilimuomba tuvute subira” alisema Ambola. Mzee Pafect aligeuka akamtazama kwa sekunde kadhaa halafu akauliza.

“Unampenda Gosu Gosu”

“Hapana” alijibu Ambola bila kupepesa macho.

“Good.Nilidhani tayari ulikwisha zama penzini.” alisema mzee Perfect.

“Ninafahamu nilikuwa kazini na siwezi kuharibu misheni kwa kuanguka penzini hivyo mapenzi yote niliyomuonesha nilikuwa naigiza”alisema Ambola.

“Gosu Gosu hafahamu wewe ni nani na kama ulikuwa kazini. Tumekuficha kwa

sababu akigundua ulikuwa unamdanganya atakuua. Taarifa zake zinaonesha ni mtu mkatili sana” alisema mzee Perfect.

“Perfect kuna kitu nahitaji unifahamishe.” Alisema Ambola huku akijisogeza karibu na mzee yule. Mwili wake wa moto ulimsisimua mzee Perfect.

“Niliwambiwa Gosu Gosu aliharibu kazi aliyotumwa Arusha ndiyo maana lilifanyika igizo lile nikaonekana nimetekwa na watu wanaotaka

kuniua ili kumshinikiza aeleze ukweli. Unaweza ukaniambia nini hasa kilichotokea huko Arusha? aliuliza Ambola.

Mzee Perfect alimtazama Ambola kwa makini kisha akasema.

“Ambola kwa usiku huu tuachane na mambo hayo ya Gosu Gosu. Nimekuja hapa kustarehe nawe hivyo naomba tutumie muda mwingi katika kujipa raha”

“Pefrect ninahitaji sana kufahamu. Naomba unieleze mpenzi wangu. Nini hasa

kilitokea? Aliuliza Ambola. Sauti ile laini ilimalinisha mzee Pefect akaamua kumueleza Ambola ukweli wote wa kile kilichotokea Arusha.

“Mungu wangu ! Kumbe Mathew ni mpelelezi! Sikulifahamu hili.Ninamfahamu kuwa ni mfanyabiashara” aliwaza Ambola baada ya mzee Perfect kumueleza kila kitu kilichotokea Arusha.

“Huyo mtu ambaye umesema ni hatari sana

anayeshirikiana na Gosu Gosu amekwisha patikana? Ambola aliuliza.

“Mathew Mulumbi bado hajapatikana lakini anaendelea kutafutwa kila kona ya nchi. Nilipaswa kuwepo katika kikao muhimu usiku wa leo ili kujua kile kinachoendelea lakini sikuhudhuria nikaja hapa kustarehe nawe. Umeiteka akili yangu Ambola.Nadhindwa hadi kufanya mambo mengine ya maana ninakimbilia kwako” alisema mzee Prfect.

“Unawaza nini malaika wangu? Aliuliza mzee Perfect.

“Nimeingiwa na hofu kwa haya uliyonieleza. Najiona kama siko salama” alisema Ambola

“Ndiyo maana uko hapa mafichoni wakati tunalishughulikia suala la usalama wako.” Alisema mzee Perfect na kumtazama Ambola kwa macho ya wasi wasi kidogo.

“Mbona unanitazama hivyo Perfect? Aliuliza Ambola.

“Kuna jambo ambalo hukupaswa kulifahamu lakini inanilazimu nikueleze.” Alijibu mzee Pefrect, akavuta pumzi ndefu.

“Jambo gani hilo Perfect? Ambola aliuliza.

“Jitihada za kumsaka Mathew Mulumbi zinaendelea hivi saa.Mara tu akatapopatikana yeye na Gosu Gosu watauawa. Baada ya hapo utakuwa huru kundelea na maisha yako kama kawaida. Hii ni siri nimekuibia. Hukupaswa kufahamu”

alisema mzee Perfect. Ambola alishitushwa na taarifa ile lakini alijitahidi kujikaza ili mzee yule asiuone mshituko wake.

“Hilo litakuwa jambo jema. Nimechoka kujificha ndani ninataka kuendelea na maisha yangu ya kawaida.” Alisema Ambola.

“Usihofu Ambola. Maficho haya ni kwa muda mfupi tu kisha utarejea katika maisha yako ya kawaida. Nitahakikisha hilo linafanyika

haraka sana.Sitaki uishi maisha haya ya kujificha ficha”

“Baada ya kumalizika kwa misheni hii ya Gosu Gosu, kutakuwa na misheni nyingine? Aliuliza Ambola.

“Misheni yako kuu ilikuwa kumlevya Gosu Gosu ili aweze kutumwa Arusha kuifanya ile kazi aliyoiharibu. Baada ya hapo hauna tena kazi nyingine labda kama itajitokeza kazi ya dharura.”

“Perfect utanisamehe kwa maswali yangu lakini mimi ni kama askari mtiifu

ninayepewa amri ya kutekeleza jambo na ninalifanya bila kuhoji. Ninataka kufahamu nini hasa dhumuni la ile kazi aliyokwenda kuifanya Gosu Gosu Arusha? Watu wale aliotumwa kuwaua wana mahusiano yoyote na misheni yetu ya Congo mpya? Aliuliza Ambola.

“Ambola leo mbona una maswali mengi namna hii? Aliuliza Perfect.

“Ninahitaji kujua kile kinachoendelea. Nimetumwa kazi nikaifanya lakini bila

kujua nini hasa malengo ya kazi ile. Leo nimepata nafasi ya kuhoji naomba unieleze hata kama ni kwa ufupi na mimi nipate picha ya kile kinachoendelea. Tangu nilipotolewa kambini nikaletwa kuishi nanyi nimekuwa nikiimbiwa misheni moja tu ya Congo mpya. Nimejiuliza maswali mengi je hiki kilichofanyika kina mahusiano yoyote na mpango wetu wa Congo mpya? Aliuliza Ambola.

“Leo umeniweza. Nitakueleza japo kwa kifupi” alisema Perfect

“Misheni ya Congo mpya haiwezi kufanikiwa bila misheni ya Tanzania mpya kufanikiwa”

“Sijakuelewa Perfect. Una maanisha nini unaposema Tanzania mpya? Kuna misheni nyingine ya Tanzania mpya? Ambola aliuliza

“Ndiyo ipo misheni ya Tanzania mpya.Tunataka kukiondoa chama kilichopo madarakni na kukiweka

madarakani chama kingine. Mpango huo ukifanikiwa ndio utakaozaa Congo mpya. Hii ni sababu tumekuwa na mashirikiano na viongozi wa operesheni yenu ya Congo mpya. Rais wa Congo Jenerali Salvatory Mamba si rahisi kumtoa madarakani kwa sababu amekita mizizi imara na wananchi wanamuunga mkono. Njia ya kutumia machafuko mpaka sasa haijazaa matunda badala yake imezidi kuzalisha wakimbizi zaidi. Umeandaliwa mpango mpya wa siri wa kumuondoa

ambao utatekelezwa pale itakapozaliwa Tanzania mpya. Huo ndio mpango tunaoendelea nao hivi sasa” alisema Perfect.

“Hapo nimeanza kukuelewa. Lakini bado nina swali. Mna hakika mpango huo utafanikiwa? Ni vipi kama mkishindwa kufanikiwa kukiondoa madarakani chama kinachotawala? Aliuliza Ambola. Mzee Perfect alitoa kicheko kikubwa.

“Ambola umenifanya nicheke kicheko kikubwa. Huu

ni mpango ambao hauwezi kushindwa. Ni mpango ulioandaliwa kwa muda mrefu na unafanyika kitaalamu sana. Hatubahatishi. Tuna uhakika asilimia mia moja tutafanikiwa ndiyo maana tunamsaka yule mwanamke ambaye anataka kuharibu mpango huu kwa kuvujisha siri.” Alisema Perfect

“Yule mwanamke aliwezaje kufahamu siri hii kubwa? Aliuliza Ambola

“Kuna mahali palitokea mwanya hadi siri hii ikamfikia

Regina. Hata hivyo siku zake zinahesabika. Ndani ya siku mbili hizi atakuwa ameuawa”

“Unaweza ukaniambia nini mnakusudia kukifanya kuhakikisha mpango wenu huo unafanikiwa? Aliuliza Ambola.

“Kwa hilo siwezi kukuambia chochote kwa sababu tumekula kiapo kutokuitoa siri hiyo. Fahamu tu kwamba mpango huo utafanikiwa na ndio utakaozaa Congo mpya. Ambola maswali yametosha natakiwa kuondoka hapa baada ya saa moja hivyo

naomba mzunguko mmoja kabla sijaondoka” alisema mzee Perfect.

Ambola hakupoteza muda. Alifanya utundu akamuamsha mzee Perfect na kumuingiza katika mzunguko lakini mzunguko uliishia kati kati baada ya simu ya Perfect kuita. Alinyoosha mkono akaichukua akatazama mpigaji mara ikulu kukapoa ghafla.

“Perfect? Alisema Ambola.

“Mke wangu anapiga. Nisipoipokea simu atahisi niko

sehemu” alisema Perfect akainuka akaipokea simu.

“Hallow” alisema Perfect halafu Akakaa kimya kumsikiliza mpigaji.

“Sikuweza kuhudhuria, nimeharibikiwa na gari. Nimemuita fundi yupo analishughulikia” alisema Perfect halafu akawa kimya kumsikiliza mpigaji. Baada ya muda akauliza.

“Wanakuja usiku huu? Aliuliza akionekana kushangaa halafu haraka haraka akaenda katika meza akachukua

kalamu na karatasi akaanza kuandika . Alipomaliza aliweka kalamu chini.

“Sawa ninakwenda mara moja kuwapokea. Nadhani nitawahi kabla ndege haijatua” alisema Perfect halafu akaendelea kumsikiliza mpigaji.

“Kila kitu hotelini kimeshamalizwa? Aliuliza Perfect. Baada ya muda akasema

“Sawa ninakwenda huko sasa hivi” alijibu na kukata simu akamgeukia Ambola.

“Mke wangu ameniambia kuna wageni muhimu wanawasili usiku huu hivyo natakiwa nikawapokee uwanja wa ndege.” Alisema halafu haraka haraka akaingia bafuni kuoga. Akiwa bafuni Ambola aliisogelea karatasi ile aliyoandika Perfect akaipiga jicho. Ilikuwa ni namba ya ndege wanayokuja nayo wageni hao pamoja na majina yao. Haraka haraka aliyanakiri majina yale katika karatasi nyingine akaificha. Perfect alitoka bafuni haraka haraka akavaa mavazi yake.

“Ambola nina haraka sana nataka niwahi wageni kabla ndege haijatua. Kesho kama nitapata nafasi nitakuja. Hapa uko salama usihofu. Kila kitu unachokitaka utakipata. Kitu muhimu usitoke nje watu wakakuona kama kuna kitu unahitaji mtume msaidizi wako atakuletea. Kama kuna tatizo lolote kubwa utanijulisha moja kwa moja” alisema Perfect na kumkumbatia Ambola akambusu. Alitoka nje akaingia katika gari lake akafunguliwa geti na walinzi

wawili wa kimasai akaondoka. Mara tu baada ya Perfect kuondoka Ambola alikwenda katika chumba cha mtu aliyepewa kumlinda na kumsaidia akagonga mlango ukafunguliwa.

“Ambola unasemaje” alisema Jackline.

“Jackline ninahitaji kuzungumza nawe jambo Fulani la muhimu”

“Kuna kitu unahitaji nikakuchukulie usiku huu? Aliuliza Jackline.

“Hapana kuna jambo nataka tuzungumze”alisema Ambola na kumtaka Jackline amfuate chumbani kwake.

“Kuna tatizo lolote Ambola? Aliuliza Jackline huku akimtazama Ambola kwa macho yake yaliyojaa umakini mkubwa.

“Jackline uko hapa kunilinda, right? Aliuliza Ambola

“Ndiyo niko hapa kuhakikisha unakuwa salama na unapata kila

unachokihitaji.” Alijibu Jackline

“Good. Unalipwa kiasi gani kwa kazi hiyo? Aliuliza Ambola.

“Masuala ya pesa ni makubaliano yangu na mtu aliyenipa kazi hii” alijibu Jackline.

“Sawa.Let’s make this simple” alisema Ambola akaenda katika kabati la nguo akalifungua na kutoa sanduku dogo akalifungua akatoa mabunda saba ya noti akayaweka mezani.

“Seven million” alisema Ambola huku akimtazama Jackline.

“Ni kwa jili ya nini hizi fedha? Aliuliza Jackline.

“Ni zako. ”

“Zangu? Kivipi? Aliuliza Jackline

“Ndiyo ni zako. I need you to do something for me”

“Nini unataka nikufanyie?

“Nataka unipeleke sehemu Fulani lakini bila waliokupa

kazi hii kufahamu” alisema Ambola.

“Usiku huu? Aliuliza Jackline.

“Ndiyo”

“Lakini maelekezo niliyopewa hutakiwi kutoka mahali hapa hadi kwa maelekezo maalum” alisema Jackline.

“Nafahamu lakini hii ni kwa mimi na wewe tu. Hakuna atakayejua”

“Ni vipi kama yule mzee atarudi tena halafu akakukosa?

“Yule mzee hatarejea tena. Tafadhali naomba unipeleke huko ninakotaka kwenda ni muhimu sana” alisema Ambola. Jackline alifikiri kidogo akayaelekeza macho mezani halafu akauliza.

“Unakotaka kwenda ni sehemu hatarishi?

“Hapana si sehemu hatarishi” alijibu Ambola. Jackline alichukua bunda moja la noti kati ya yale mabunda saba halafu akasema.

“Weka hizo fedha zako. Hizi zinanitosha. Jiandae

nitakupeleka huko unakohitaji” alisema Jackline.

“Ahsante.” alisema Ambola na kuzirejesha fedha katika sanduku lake akaanza kujiandaa. Baada muda mfupi alikuwa tayari amejiandaa akatoka akamfuata Jackline ambaye tayari alikwisha andaa gari wakaingia. Mlinzi wa kimasai alifungua geti wakatoka. Ambola alimuelekeza mahali wanakoenda. Jackline hakuonekana kutaka

mazungumzo hivyo safari ilikuwa ya kimya kimya.

“Ninacheza na watu wabaya sana. Perfect na mtandao wake ni watu hatari mno. Ninapaswa kuwa nao makini . Hawa ni wale vibaraka wa mabeberu. Ni wale ambao wanatumiwa kuzihujumu nchi zao wenyewe. Hawana huruma na maisha ya watanzania wanachokihitaji wao ni kutimiza malengo ya mabeberu.” Aliwaza Ambola.

“Kwa sasa nimeifahamu mipango yao japo bado sijajua

ni namna gani wamepanga kukiondoa madarakani chama kinachotawala ili wakiweke chama wanachokitaka wao. Nadhani huu ni wakati muafaka kabisa wa kuingia katika mapambano ya kuipigania nchi yangu Tanzania. Nadhani baba aliniandaa kwa ajili ya wakati kama huu. Baba yangu alikuwa mzalendo na alikubali kufa kuliko kuwaacha mabeberu kuwa na siri za utajiri wa nchi yetu. Wakati ule sikuelewa sana nini maana ya uzalendo kwa nchi lakini kwa sasa baada

ya kuwa mkubwa na kwa mambo niliyoyapitia nina haki ya kumsifu baba yangu kwa ushujaa mkubwa aliouonesha kwa nchi yake. Nitahakikisha siku moja jina lake linaandikwa katika orodha ya mashujaa wa nchi hii. Hata hivyo bado kuna mengi nahitaji kuyafahamu kuhusu baba, alikuwa jasusi au aliwezaje kuzipata ramani zile? Hilo litakuja baadae kwa sasa natakiwa kushughulika na hiki kinachoendelea. Hawa jamaa bado hawajanigundua kama mimi ni mtanzania.

Wanaamini mimi ni raia wa Congo. Natakiwa kuitumia vyema nafasi hii kabla sijajulikana kuhakikisha mtandao huu wote unafumuliwa na mipango yao yote haifanikiwi. Hili linatakiwa kufanyika haraka sana kabla ya uchaguzi mkuu .” Aliwaza Ambola na kufuta machozi kwa kutumia kiganja chake cha mkono. Aliwaza kwa hisia kali mno.

“Ambola una tatizo gani? Mbona unalia? Aliuliza Jackline

“Niko sawa usijali” alijibu Ambola akakiegemeza kichwa chake katika kioo cha dirisha.

“Natakiwa kumtafuta na kuonana na Mathew Mulumbi. Perfect ameonesha woga mkubwa kuhusu huyu mtu. Wameingiwa na hofu baada ya Gosu Gosu kumshirikisha katika mauaji ya kule Arusha ndiyo maana wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wanampata na kumuua. Huyu hasa ndiye ninayepaswa kumsaka na kumpata. Ili nimpate Mathew Mulumbi

lazima kwanza nionane na Gosu Gosu. Natakiwa kujua mahali aliko na kumsaidia kumtoa katika mpango wa kumuua. Nikichelewa hawa mashetani wanaweza wakamuua. Wamemficha mahali pa siri. Lazima nimtafute na kuhakikisha nimempata. Mafunzo yote niliyoyapitia wakati wa kuyatumia ni sasa" aliwaza Ambola.

"Thomas ndiye aliyenipa wazo la kuanzisha mahusiano na mzee Perfect. Nililikataa

wazo hili lakini alinisisitiza kuwa siku moja litakuwa na manufaa na sasa nimeanza kuyaona manufaa yake. Kama nisingekuwa katika mahusiano na mzee yule ningepata ugumu sana katika kuzifahamu siri zao. Japokuwa sifurahii mahusiano hayo lakini yana faida. Hata hivyo napaswa kuwa makini sana na yule mzee.” Aliendelea kuwaza Ambola.

Jackline alifuata maelekezo aliyopewa akafika hadi katika nyumba moja.

Ambola alishuka akatazama kila upande kama kuna mtu halafu akaenda getini. Alibonyeza kengele mara tatu. Baada ya sekunde chache iliwaka taa yenye mwangaza mkali halafu ikazima. Haukupita muda geti likafunguka. Ambola akamtaka Jackline aingize gari ndani na amsubiri garini. Moja kwa moja Ambola alielekea katika mlango wa kuingilia sebuleni. Alisimama kwa sekunde chache halafu mlango ukafunguliwa.

“Ambola ingia ndani” alisema Thomas Ngalula. Sura yake ilionesha wasiwasi mwingi.

“Kuna nini usiku huu? Nani yule umekuja naye? Aliuliza Thomas.

“Usihofu Thomas. Yule ni Jackline ambaye amepewa jukumu la kunilinda na kuhakikisha ninapata kila ninachokihitaji. ” Alisema Ambola.

“Una hakika hataweza kuvujisha siri kuwa ulikuja hapa? Sitaki watu wajue kama

mimi nawe tuna mahusiano” alisema Thomas.

“Thomas usiwe na hofu yoyote. Niamini tafadhali. ” Alisema Ambola. Thomas alifunua pazia kidogo akatazama nje halafu akamgeukia Ambola.

“Twende huku tafadhali” alisema Thomas. Ambola alimfuata hadi katika chumba kitupu.

“Haya nieleze kuna nini usiku huu? Kabla hujasama chochote nataka unihakikishie kwamba hamkuwa

mnafuatiliwa” alisema Thomas.

“Hakuna aliyekuwa anatufuatilia Thomas usihofu”

“Lazima nihofu Ambola. Kitendo cha mimi kuonekana niko nawe ni hatari kubwa kwetu na mipango yetu yote inaweza ikaharibika.”

“Thomas nimechukua kila aina ya tahadhari kuhakikisha kuja kwangu hapa hakutaleta matatizo kwetu” alisema Ambola

“Pamoja na hayo zingatia hili. Kuanzia sasa usimuamini mtu yeyote ambaye anashirikiana na hawa watu. Kosa dogo sana linaweza kuharibu misheni ambayo imechukua miaka kuiandaa. Umenielewa Ambola?”

“Nimekuelewa Thomas”

“Vizuri. Haya nieleze kwa nini umekuja hapa usiku huu? Aliuliza Thomas.

“Thomas nimelazimika kuja kwako usiku huu kwa sababu wakati umefika wa kuifanya ile kazi ambayo

umekuwa unaniambia baba alinitaka niifanye. Nilikuwa na mzee Perfect usiku huu” Ambola alimueleza Thomas kila kitu alichoambiwa na Perfect.

“Umeufanya mwili wangu wote usisimke.” Alisema Thomas baada ya Ambola kumueleza kila kitu.

“Mimi pia. Ndiyo maana nimeamua kuja usiku huu kukuletea taarifa hizi. Muda umefika wa mimi kuifanya kazi ya kuusambaratisha mtandao huu. Kwanza kabisa nataka

kufahamu mahali alipo Gosu Gosu. Sitaki auawe.” Alisema Ambola.

“Ambola sikushauri ufanye lolote kuhusu Gosu Gosu kwa sasa. Umakini mkubwa sana unatakiwa katika jambo hili. Ukiteleza kidogo na hawa jamaa wakakugundua, umekwisha. Kila kitu kitaishia hapo. Nakushauri achana na Gosu Gosu” alisema Thomas.

“Siwezi kumuacha Gosu Gosu akauawa. Ni mimi niliyemuingiza katika masahibu haya anayoyapitia

hivi sasa hivyo lazima nihakikishe ninamuokoa. Siko tayari Gosu Gosu auawe. Dhumuni lingine la kumuokoa Gosu Gosu ni kumpata Mathew Mulumbi. ”

“Mathew Mulumbi” alisema Thomas.

“Ndiyo. Natakiwa kumpata Mathew Mulumbi. Huyu ni rafki mkubw wa Gosu Gosu na sikujua kama ni mpelelezi mashuhuri.Nimeuona woga mkubwa katika sura ya Perefect wakati akilitamka jina hilo. Mathew ndiye mtu sahihi

kushirikiana naye lakin hatuwezi kujua mahali alipo bila ya kumtumia Gosu Gosu.” Alisema Ambola.

“Si wazo baya lakini wazo la kutaka kumuokoa Gosu Gosu mimi bado sikubaliani nalo. Linaweza kutuletea matatizo. Hawa watu wameamua kukupeleka mafichoni ili kukuepusha na Gosu Gosu. Kwa sasa anachofahamu tayari umekufa au unashikiliwa sehemu fulani. Hapaswi kufahamu unashirikiana na hawa watu na

wewe ni sehemu ya waliofanikisha mpango wa kumtumia yeye kufanya mauaji jijini Arusha.” Alisema Thomas.

“Thomas, lazima nionane na Gosu Gosu. Nina uhakika mkubwa sana nikionana nay…. ”Ambola alikatishwa na Thomas.

“Ambola nisikilize ninachokwambia. Mimi nina uzoefu mkubwa katika haya mambo zaidi yako. Ukionana na Gosu Gosu utamweleza nini? Alioneshwa lile igizo

ukiwa umefungwa mahali unateswa na ukatishiwa kuuawa kama asipoonesha mahali alipo Mathew Mulumbi. Utamwambia umetokaje katika mikono ya wale waliokuwa wanakushikilia? Mpaka sasa Gosu Gosu anaamimi wewe ni mtoto wa Bernadetha na mzee Perfect, utamweleza nini atakapokuuliza kwa nini mama yako alitaka kukuua? Aliuliza Thomas. Ambola alikaa kimya kidogo

“Thomas hebu niambie kuna namna yoyote ya kuweza kumpata Mathew Mulumbi bila ya kumtumia Gosu Gosu? Aliuliza Ambola

“Simfahamu Mathew Mulumbi na sifahamu ni namna gani tutaweza kumpata lakini bado suala la kumuokoa Gosu Gosu sikubaliani nalo.Litavuruga mambo mengi”

“Thomas ni wewe uliyesimama nami hadi dakika hii. Hujawahi kuniacha hata mara moja. Ulitumia muda

mrefu kuniandaa kwa ajili ya misheni hii. Hata hawa jamaa nao wametumia muda mrefu kuandaa misheni yao na umefika muda wa kutekeleza mipango yao. Wanaanza na hapa Tanzania kama alivyosema Perfect halafu watahamia Congo. Na sisi pia umefika muda wetu wa kutekeleza misheni yetu. Ninaomba tafadhali unisaidie niikamilishe misheni hii" alisema Ambola.

"Nini unahitaji nikusaidie Ambola?

“Nahitaji kufahamu mahali alipo Gosu Gosu. Mambo mengine niachie mimi nitajua nini cha kufanya. Nakuahidi sintaharibu chochote” alisema Ambola. Thomas alitafakari kwa muda halafu akaema.

“Sawa nitakusaidia kujua mahali alipo Gosu Gosu. ” Alisema Thomas akanyamaza kidogo.

“Kuna mtu mmoja ambaye anaweza kutusaidia kujua mahali alipo Gosu Gosu ambaye ni Joseph Tshibanga.

Huyu nitaonana naye kesho. Nitajaribu kumshawishi anieleze mahali alipo Gosu Gosu. ”

“Ninashukuru sana Thomas kwa kukubali kunisaidia lakini suala hili lazima likamilike usiku huu wa leo. Hawa jamaa wanaweza wakamuua Gosu Gosu wakati wowote.” Alisema Ambola.

“Ambola usiwe na haraka katika jambo hili. Tukienda kwa haraka kama unavyotaka tutajikuta tumeharibu kila kitu” alisema Thomas.

“Thomas hatuna muda wa kusubiri. Mambo lazima yaanze. Tukichelewa tutakosa kila kitu” alisisitiza Ambola. Thomas alifikiri kwa muda halafu akachukua simu yake akaitafuta namba ya Joseph Tshibanga akampigia. Simu iliita na kupokelewa.

“Hallow Thomas. ”Alisema Joseph.

“Joseph uko wapi muda huu? Aliuliza Thomas baada ya kusikia kelele nyingi za watu wakishangilia.

“Nipo katika onesho la mwanamuziki Banze Mbumba kutoka Kinshasa. Kwa nini hujafika hapa? Karibu wacongo wote wako hapa” alisema Joseph.

“Sikuwa na habari kama Banze Mbumba ana onesho leo Dar es salaam. Ninakuja hapo sasa hivi nina jambo pia ninahitaji kuzungumza nawe? Alisema Thomas na kukata simu.

“Ambola ninakwenda kuonana na Joseph. Yeye lazima anafahamu mahali

alipo Gosu Gosu na hata kama hafahamu ni yeye mwenye ukaribu na mtandao wa Tanzania hivyo anaweza akauliza na akajua mahali alipo Gosu Gosu. Utabaki hapa wewe na mwenzako. Tafadhali usimfungulie mlango mtu yeyote hadi nitakaporejea” alisema Thomas akaelekea chumbani kwake akachukua bastola akaifunga kiwambo cha kuzuia sauti akaificha katika koti akaelekea katika gari lake na kuondoka.

“Twende ndani Jackline. Ninamsubiri yule jamaa atarejea muda si mrefu” Ambola alimwambia Jackline aliyekuwa garini akimsubiri. Jackline alitazama saa yake halafu akafungua mlango akamfuata Ambola wakaelekea sebuleni.

“Ambola hatupaswi kuchukua muda mrefu mahali hapa. Nina hofu anaweza akatokea yule mzee wako akakukosa. Lawama zote zitaniangukia mimi na

nitakuwa nimepoteza kazi yangu” alisema Jackline.

“Usihofu Jackline hatutachukua muda mrefu. By the way unatumia kinywaji gani?

“Kinywaji chochote kikali kama kipo nitatumia” alijibu Jackline. Ambola aliifahamu vyema nyumba ya Thomas kwani amekuwa akienda mara kwa mara.Alienda moja kwa moja katika kabati ambamo Thomas huhifadhi vinywaji akachukua chupa ya pombe kali halafu akaenda katika friji

akachukua chupa mbili za soda akaweka mezani. Jackline aliichukua chupa ile ya mvinyo akaitazama halafu akatabasamu.

“Wow ! Johnnie Walker Blue label.” Alisema Jackline huku akitabasamu.

“Umewahi kuutumia mvinyo huu? Aliuliza Ambola. Jackline alitoa kicheko kidogo huku akimimina mvinyo ule katika glasi.

“Nina utaalamu mkubwa katika idara hii ya vinywaji.” Alijibu Jackline. Aliinua glasi

akapiga funda kubwa halafu akamtazama Ambola.

“Huyu jamaa anaishi mwenyewe? Aliuliza.

“Ndiyo anaishi mwenyewe. Mke wake kwa sasa anaishi Ufaransa na ndiye humtumia mvinyo huu mkali” alijibu Ambola.

“Jackline wewe ni mwenyeji wa wapi? Aliuliza Ambola baada ya kupiga funda moja. Kabla ya kujibu Jackline aliinua glasi akapiga funda lingine.

“Ninatokea mkoa wa Kilimanjaro. Wewe unatokea wapi? Aliuliza Jackline.

“Mimi natokea Congo”

“Congo? Jackline alishangaa.

“Ndiyo. Mbona umeshanga?

“Nimeshangaa kwa sababu lafudhi yako haifanani na watu wa kutoka Congo.” Alisema Jackline.

“Ni kwa sababu nimekulia hapa Tanzania. Nimekuja hapa nikiwa na miaka nane na sasa

nina miaka zaidi ya ishirini.”alisema Ambola

“Nini hasa sababu ya kuondoka Congo? Aliuliza Jackline

“Machafuko. Vita.” alijibu Ambola kwa kifupi.

“Ndugu zako bado wako Congo? Aliuliza Jackline akainua glasi akapiga funda lingine.

“Sina ndugu kwa sasa. Wote wameuawa”

“Dah ! pole sana” alisema Jackline.

“Jackline tuachane na hayo ya Congo. Hapa jijini unajishughulisha na nini?

“Biashara na wakati mwingine kazi kama hizi.”

“Ulinzi? Ambola aliuliza.

“Ndiyo”

“Umepitia mafunzo ya kijeshi au mafunzo yoyote ya kujihami? Ambola aliuliza.

“Hapana sijapitia mafunzo yoyote ya kijeshi au ya kujihami ila nimepitia mafunzo ya silaha.Ninaweza

kuchezea vizuri silaha yoyote” alijibu Jackline

“Ikawaje ukapewa kazi ya kunilinda ilhali hujapitia mafunzo ya ulinzi? Aliuliza Ambola. Jackline alipiga funda la kinywaji akatabasamu kidogo halafu akaitoa bastola yake akaiweka mezani.

“Unanionaje, siwezi kukulinda? Aliuliza.

“Simaanishi hivyo.” Alijibu Ambola.

“Sikiliza Ambola. Hadi nimepewa kazi ya kukulinda

mtu kama wewe nimeaminiwa vya kutosh hivyo usiwe na wasi wasi wowote. Nitahakikisha unakuwa salama. Usiwe na hofu yoyote ukiwa nami" alisema Jackline.

"Sina hofu hata kidogo." Alisema Ambola.

Kila mmoja aliinua glasi akapiga funda la kinywaji.

"Hapa mjini unajishughulisha na nini? Jackline aliuliza.

"Ninajishughulisha na biashara mbali mbali"

“Good. Mimi pia ninafanya bisahara. Ninajishughulisha na biashara ya madini na zikitokea kazi kama hizi ninafanya. Sichagui kazi. Ninachohitaji ni pesa iingie mfukoni” alisema Jackline. Kilipita kimya kifupi.

“Jackline kama hutajali unaweza ukaniambia kiasi gani unalipwa na waliokupa kazi ya kunilinda? Aliuliza Ambola.

“Hii ni mara ya pili unaniuliza swali kama hilo. Kwa nini unataka kufahamu? Aliuliza Jackline akainua tena

glasi yake akapiga funda kubwa. Glasi lilibaki tupu akamimina mvinyo mwingine.

“Ninataka kufahamu kwa sababu ninataka kukununua ili unifanyioe kazi yangu.” Alisema Ambola.

“Kuninunua? Jackline alishangaa.

“Ndiyo.Ninataka kufanya hivyo ili unifanyie kazi yangu bila ya waajiri wako kujua” alijibu Ambola na kumtazama Jackline.

“Nitakulipa mara mbili au tatu ya kiasi unacholipwa.Unasemaje? aliuliza Ambola.

“Nnalipwa laki tano kukulinda kwa siku moja.” Alisema Jackline.

Ambola alipiga funda akamtazama Jackline.

“Mimi nitakulipa zaidi ya hapo” alisema Ambola.

“Ni kazi gani unataka nikufanyie? Jackline aliuliza.

“Nitakwambia tutakaporejea nyumbani.”

“Ni kazi ya kutumia silaha? Aliuliza Jackline.

“Ndiyo inaweza ikahusisha silaha”

“Good.Ninainyanyasa bunduki yoyote au bastola vile nitakavyo” alisema Jackline.Ambola akatabasamu.

“Good. Tutazungumza zaidi baadaye”

****

Thomas Ngalula aliwasili katika ukumbi mkubwa wa burudani maarufu kama jumba jeupe. Watu walifurika katika onesho la mwanamuziki Banze Mbumba kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo. Alimtumia Joseph ujumbe mfupi wa simu akamjulisha kuwa tayari

amefika pale ukumbini. Joseph alimjibu kwa ujumbe mfupi akamtaka wakutane nje. Thomas alielekea mahali ambako Joseph alielekeza wakutane. Aliagiza bia akaipeleka mdomoni na alipoiweka chini tayari ilikuwa nusu.

“Thomas” ilisema sauti nyuma yake.Alikuwa ni Joseph.

“Karibu Joseph.Samahani kwa usumbufu” alisema Thomas akitumia lugha ya Lingala.

Joseph aliagiza bia halafu akamtaka Thomas wahame pale kaunta waelekee katika meza ambayo haikuwa na mtu.

“Hukujua kama Banze Mbumba ana onesho leo? Joseph aliuliza.

“Hapana sikufahamu kama kuna onesho la Banze Mbumba” alijibu Thomas.

“Kuna tatizo gani usiku huu Thomas ? Aliuliza Joseph.

“Joseph nimekuja kuzungumza nawe jambo moja muhimu sana.”

“Jambo gani Thomas?

“Ni kuhusiana na misheni yetu inayoendelea ya Congo mpya.” Alisema Thomas.

“Nakusikiliza”

“Nimeanza kuwa na wasi wasi sana na hawa watu wa Tanzania tunaoshirikiana nao.” Alisema Thomas

“Kwa nini una wasiwasi nao? Aliuliza Joseph.

“Nimepata taarifa usiku huu kwamba wana mpango wa kumuua Gosu Gosu pale

watakapompata Mathew Mulumbi” alisema Thomas.

“Kumuua Gosu Gosu? Joseph alishangaa.

“Ndiyo wana mpango huo wa kumuua”

“Kwa nini wanataka kumuua wakati hatujakubaliana hivyo? Umezipata wapi taarifa hizi? Aliuliza Joseph.

“Unakumbuka niliwahi kukushauri kuwa tumtumie Ambola kuwachunguza hawa watu tunaoshirikiana nao.Basi

taarifa hiyo nimeipata kwa Ambola.Ameambiwa na Perfect.”

Joseph alimtazama Thomas kwa sekunde kadhaa halafu akatoa pakiti ya sigara akachomoa moja akaiwasha akavuta.

“Umenishitua sana Thomas.Una uhakika na taarifa hiyo kutoka kwa Ambola? Aliuliza Joseph.

“Nina uhakika nayo. Mzee Perfect ameleweshwa mapenzi na Ambola.Yuko tayari kumueleza siri zote” alisema

Thomas. Joseph alizama katika tafakari.

“Joseph lazima tumuokoe Gosu Gosu.Yule ni mtu wetu muhimu sana katika misheni hii.Hatuwezi kukubali mtu wetu akauawa.”

“Uko sahihi Thomas.Gosu Gosu ni muhimu katika misheni yetu.Siko tayari auawe.” Alisema Joseph.

“Unafahamu mahali alipo Gosu Gosu? Thomas aliuliza

“Hapana. Sifahamu mahali alipo lakini nitapafahamu” alisema Joseph.

“Tunatakiwa kumuokoa usiku huu.” Alisema Thomas.

“Kama tukimuokoa usiku huu hawa jamaa wanaweza wasimpate Mathew Mulumbi na kama wasipompata huyu mtu misheni yao inaweza ikaharibika.Tunawategemea wao sana.Ukamilifu wa misheni yao ndio ukamilifu wa misheni yetu” alisema Joseph.

“Joseph tunatakiwa kumuokoa mtu wetu.Hawa

watu si wazuri hata kidogo na yawezekana wanatutumia bila sisi kujua.Wamemtumia Gosu Gosu kufanya mauaji ya Arusha. Baada ya kukamilisha kazi yao, sasa wanataka kumuua kwa sababu hana tena faida kwao. Tunatakiwa kumjali mtu wetu.Tukiruhusu Gosu Gosu akauawa unadhani nani atafuata kesho? Unaweza kuwa wewe.” Alisema Thomas.Joseph alikunywa bia yake halafu akasema.

“Uko sahihi Thomas. Hata mimi kuna chembe chembe za

usaliti nimeziona tayari.Ahsante sana kwa kunifumbua macho.” Alisema Joseph ambaye alionekana kulemewa na kilevi.Alitoa simu akaitafuta namba ya Bernadetha akampigia.

“Thomas unasemaje ? Aliuliza Bernadetha baada ya kupokea simu.

“Bernadetha samahani kwa usumbufu”

“Bila samahani.Kuna nini usiku huu?

“Mathew Mulumbi tayari amepatikana? Aliuliza Joseph.

“Nimepokea taarifa kutoka kwa timu iliyotumwa kwenda mahali alikoelekeza Gosu Gosu lakini hawajafanikiwa kumpata Mathew”

“Bernadetha ninataka kuzungumza tena na Gosu Gosu. Naamini nikizugumza naye anaweza akafunguka zaidi mahali aliko Mulumbi”

“Hilo ni wazo zuri sana. Uko wapi Joseph?

“Nielekeze ulipo nikufuate unipeleke alipo Gosu Gosu nikazungumze naye” alisema Thomas.Bernadetha alimpa maelekezo mahali alipo.

“Umekuja na gari? Joseph aliuliza

“Ndiyo.” Alijibu Thomas.

“Twende” alisema Joseph huku akisimama na kumalizia bia yake.Waliingia katika gari la Thomas wakaondoka.

“Tutamuokoaje Gosu Gosu? Aliuliza Thomas.

“Unayo bastola? Aliuliza Joseph.

“Ndiyo ninayo”

“Safi.Naiomba.Mimi sijatembea na silaha yoyote leo” alisema Joseph.Thomas aliitoa bastola yake katika koti akampatia Joseph.

Walifika mahali walikopanga wakutane.Joseph alimpigia simu Bernadetha ambaye alitoka katika ile hoteli alikokuwa akaingia katika gari la Thomas wakaondoka kuelekea mahali aliko Gosu Gosu.

“Lazima Mathew apatikane usiku wa leo” alisema Joseph baada ya kimya kutawala garini.

“Ni Gosu Gosu pekee ambaye anaweza akatusaidia kumpata.Mathew ni mtu wake wa karibu sana” alisema Bernadetha.

“Usihofu kuhusu hilo.Ataeleza kila kitu” alisema Joseph.

Walifika katika nyumba alimo Gosu Gosu.Geti lilifunguliwa na walionekana watu wanne wakiwa wamekaa

mahali wakizungumza.Mmoja wa wale jamaa alimpokea Bernadetha akamuongoza kuelekea ndani. Gosu Gosu alikuwa amefungwa katika kitanda cha chuma.Mkono wake wa kulia ulikuwa umefungwa pingu iliyounganishwa na chuma cha kitanda.

“Mfungueni” alisema Joseph huku akiitoa bastola.Yule jamaa aliyeongozana nao alitoa ufunguo wa pingu akaifungua Gosu Gosu akawa huru.

“Joseph mnataka nini tena? Mathew amepatikana? Aliuliza Gosu Gosu.

“Mathew hajapatikana.Tumekuja hapa ili utuoneshe mahali alipo.” Alisema Joseph huku akimnyooshea Gosu Gosu bastola.

“Josep…” alisema Gosu Gosu kwa mshangao lakini ghafla Joseph aligeuka akaachia risasi mbili zilizokifumua kichwa cha yule mlinzi waliyekuwa naye mle chumbani.Bernadetha

alipatwa na mshangao mkubwa.Hakutegemea.

“Joseph nini umefanya? Aliuliza.

“Ulikosea sana Bernadetha kutaka kutuzunguka.” alisema Joseph.

“Joseph sikuelewi una maanisha nini? Aliuliza Bernadetha huku akitetemeka.

“Tunafahamu mpango wenu wa kumuua Gosu Gosu pale mtakapompata Mathew Mulumbi.Huo ni usaliti mkubwa sana

Bernadetha.Hatuwapi nafasi hiyo ya kumuua mtu wetu.”

“Joseph ! umetoa wapi taarifa hiyo? Aliuliza Bernadetha huku akitetemeka.Mara suruali ya jeans aliyovaa iliiloa.Alishindwa kuizuia haja ndogo kumtoka.

Macho ya Joseph hayakuwa na hata chembe ya huruma.Kidole chake kiliizinga ile bastola aliyoishika mkononi.Risasi ilitoka katika mdomo wa bastola ikazama

katika kichwa cha Bernadetha akaanguka chini kama furushi.

“Gosu Gosu inuka tuondoke.Uko huru sasa” alisema Joseph halafu akamrejeshea Thomas bastola yake.

Kufumba na kufumbua kilitokea kitendo cha ajabu.Mkono wa Thomas uliinuliwa kwa kasi kubwa akaizinga bastola na kuachia risasi moja ambayo ilimpata Joseph katika paji lake la uso akaanguka chini.

“Hey ! alisema Gosu Gosu kwa mshangao.

“Usihofu Gosu Gosu.Sasa uko salama” alisema Thomas.

“Wewe ni nani? Aliuliza Gosu Gosu.

“Naitwa Thomas Ngalula.Niko hapa kukuokoa” alisema Thomas.

“Kuniokoa? Nani kakutuma uje kuniokoa? Kwa nini umemuua Joseph? Aliuliza Gosu Gosu.

“Gosu Gosu sihitaji maswali mengi.Kuna jamaa

watatu hapo nje ambao tunatakiwa kuwamaliza ili tuondoke mahali hapa.Mpekue huyu jamaa chukua bastola yake tumalize kazi” alisema Thomas.Gosu Gosu alimpekua yule mlinzi aliyeuliwa na Joseph akaichukua bastola yake ambayo haikuwa na kiwambo cha sauti.

“Naomba hiyo bastola yenye kiwambo cha sauti.Hii nikiitumia itatoa mlio mkubwa na itavuta watu kusogelea mahali hapa” alisema Gosu Gosu.Thomas alimpatia ile

bastola yake.Walitoka mle ndani.Waliwakuta wale jamaa watatu wakiwa wamesimama pembeni ya gari wakizungumza.Gosu Gosu aliwadonoa vichwa vyao kwa risasi wote wakaanguka chini.

“Una hakika hakuna wengine? Aliuliza Gosu Gosu huku jicho lake likizunguka kila upande kama Kinyonga.

“Tulipoingia hapa tulikuta watu wanne pekee.Naamini hakuna wengine.Gosu Gosu tuondoke mahali hapa mara moja” alisema

Thomas.Waliingia katika gari wakaondoka.

“Wewe ni nani? Kwa nini umemuua Joseph? Aliuliza Gosu Gosu.

“Utafahamu zaidi lakini kwa kifupi yule ni msaliti na anastahili kuuawa” alijibu Thomas.Gosu Gosu alimtazama kwa makini akauliza tena.

“Wewe ni nani kwani?

“Gosu Gosu nakuahidi utafahamu kila kitu kuhusu mimi na kwa nini nimekuja

kukuokoa lakini kabla ya hapo kuna sehemu ninakupeleka ukaonane na mtu”

“Mtu? Nani huyo? Aliuliza Gosu Gosu

“Vuta subira kidogo utaonana naye.Ni mtu muhimu sana na baada ya kuonana naye utafahamu kila kitu kinachoendelea.Usiwe na hofu nami hata kidogo.Mimi ni mtu mwema.” Alisema Thomas.

“Mtu mwema wakati umemuua Joseph Tshibanga

kikatili namna ile?” Aliuliza Gosu Gosu.

“Ilikuwa lazima afe ili uwe huru.Sikukosea kumuua” alisema Thomas.

Safari iliendelea hadi walipofika nyumbani kwa Thomas.Alipiga honi kwa mtindo aliomuelekeza Ambola na baada ya dakika chache geti lilifunguliwa gari likaingia ndani.

“Tumefika” alisema Thomas akashuka garini.Gosu Gosu naye alishuka

garini.Alimfuata Thomas kuelekea ndani.

Mara tu alipoingia ndani alijikuta akifunga breki za ghafla baada ya kukutanisha macho yake na Ambola.

“Son of b……” alisema kwa hasira huku akipiga hatua kumsogelea Ambola.Sura yake ilibadilika.Macho yake yalionesha ukatili kama macho ya Simba.

“Gosu Gosu pleas…” alisema Thomas lakini alisukumwa akaanguka

chini.Hatua chache kabla ya kumfikia Ambola alisikia vyuma vya silaha vikigusana halafu sauti kali ikamuamuru.

“Stop !

Gosu Gosu aligeuka akajikuta akitazamana na Jackline aliyemnyooshea bastola.

“Huyu ni nani? Gosu Gosu alijiuliza huku akimtazama Jackline kwa makini sana.

“Piga magoti tafadhali ! alisema Jackline.Sura yake

haikuonesha masihara hata kidogo.

“Wewe ni nani wa kuniamuru mimi? Unanifahamu vizuri? Aliuliza Gosu Gosu lakini kabla hajakaa sawa zilipita risasi mbili kulia na kushoto mwa kichwa chake na kupiga ukuta.

“Ninaposema piga magoti fanya hivyo haraka sana.You have three seconds ! aliamuru Jackline.

“Huyu mwanamke ni hatari sana. Si wa kufanyia masihara hata kidogo.Ngoja

nitii anachoniamuru” aliwaza Gosu Gosu na kupiga magoti akainua mikono juu. Zilipita sekunde kadhaa Ambola akasema.

“Gosu Gosu simama na uketi pale” alisema Ambola.Gosu Gosu alimtazama Jackline halafu akamtazama Ambola akainuka akaketi sofani.

“Mwanamke huyu ni nani? Gosu Gosu aliendelea kujiuliza maswali.

“Gosu Gosu, hapa ndipo nilipokuleta na huyu ndiye

unayetakiwa kuonana naye.Naamini mnafahamiana vyema” alisema Thomas. Sura ya Gosu Gosu ilibadilika.Alimtazama Ambola kwa hasira akatikisa kichwa.

“Sikutegemea kabisa” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu una haki ya kukasirika, una haki ya kunifanya utakavyo kwa haya mambo yaliyokukuta lakini naomba unipe muda kidogo unisikilize kile ninachotaka kukueleza” alisema Ambola.

“Huna cha kunieleza Ambola.Tayari ninafahamu kila kitu kuhusu wewe.Kama ningefahamu kuwa ninakuja kuonana na nyoka kama wewe nisingekuja mahali hapa.Kwa nini Ambola ukanifanyia hivi? Aliuliza Gosu Gosu akiendelea kutazamana na Ambola.

“Huyu tayari amekwisha elezwa kila kitu.” Aliwaza Ambola

“Ambola nilikupenda kupita hata ninavyojipenda mwenyewe lakini kumbe nilizama mapenzini na chui

mwenye ngozi ya Kondoo.” Alisema Gosu Gosu huku akitaka kusimama.Jackline aliyekuwa amesimama karibu na mlango alikuwa mwepesi mno na tayari mkono wake uliokuwa na bastola ulinyanyuka.

“Ambola this is not over.Mimi nawe tutakutana tena.Ahsante kwa kila kitu” alisema Gosu Gosu.

“Naomba uketi tafadhali.! Alifoka Ambola.Gosu Gosu alimtazama kwa dharau halafu

akageuka akakutanisha macho na Jackline .

“Umesikia ulichoambiwa.Sit down ! alifoka Jackline.

“Gosu Gosu naomba uketi tafadhali usikilize kile ambacho Ambola anataka kukwambia” alisema Thomas, .

“Hana cha kuniambia huyu shetani! Alifoka Gosu Gosu.

“Kwa taarifa yako umeokolewa kutoka mahali pale kwa msaada wa huyu

Ambola.Ni yeye aliyenasa mpango wa kutaka kukuua”

“Kuniua? Gosu Gosu alishangaa.

“Kaa chini uelezwe kila kitu” alisema Thomas.Gosu Gosu alimtazama Ambola halafu akaketi.

“Nani wanaotaka kuniua? Aliuliza

“Bila kukutoa mahali pale mpango ulikuwa ni kukuua” alisema Ambola.

“Nakuuliza nani wanataka kuniua?

“Bernadetha na kundi lake.Hawana mpango wa kukuacha hai”

“Unawezaje kusema Bernadetha na kundi lake wakati wewe ni mmoja wao? Alihoji Gosu Gosu.

“I’m not one of them” alisema Ambola.

“Yes you are ! alisema Gosu Gosu kwa ukali.

“Ningekuwa sehemu yao nisingefanya mpango wa kukuokoa” alisema Ambola.

“Huna unachoweza kunidanganya Ambola.Ninakufahamu nje ndani.Wewe ni mama wa uongo.Nyoka mkubwa wewe.Ninakuchukia Ambola” alisema Gosu Gosu.Mwili ulimtetemeka kwa hasira.

“Una haki ya kukasirika na kunichukia lakini naomba unipe dakika tano tu nikwambie kitu muhimu.” alisema Ambola.

“Gosu Gosu tafadhali naomba umsikilze Ambola kwa dakika chache kisha utaamua

uondoke au vipi” alisema Thomas.

“Hebu sema haraka hicho unachotaka kukisema” alisema Gosu Gosu.

Ahsante” alisema Ambola.

“Kwanza kabisa naomba ufahamu mimi si raia wa Congo mimi ni mtanzania” alisema Ambona na sura ya Gosu Gosu ilibadilika.

“What? Jackline aliyekuwa mlangoni naye alisema kwa sauti ndogo ya mshangao.

“Ninakwambia ukweli sikudanganyi Gosu Gosu.Tafadhali endelea kunisikiliza” alisema Ambola. Alimueleza Gosu Gosu kuhusiana na kisa cha baba yake.Alieleza kilichomtokea baba yake hadi alivyofika kwa Thomas.

“Baada ya hapo ndipo nilipopelekwa na Thomas katika kambi ya wakimbizi wa kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo ambako niliandikishwa kama mkimbizi kutoka Congo”

alisema Ambola. Gosu Gosu alimtazama halafu akamtazama Thomas.

“Ni kweli anachokisema Ambola.Mimi ndiye niliyefanya mpango akapekelewa katika kambi hiyo ya wakimbizi na akatambuliwa kama raia wa Congo” alisema Thomas.

“Na wewe ni nani ? Aliuliza Gosu Gosu.

“Mimi ni Thomas Ngalulka.Ni Raia wa Congo lakini nimeishi hapa Tanzania

kwa zaidi ya miaka ishirini na tano sasa.”

“Unafanya kazi gani hapa Tanzania? Aliuliza Gosu Gosu.Thomas alimtazama Jackline akamtaka atoke nje.

“Hapana.Jackline atabaki.Anatakiwa asikilize na afahamu kila kitu tunachokizungumza” alisema Ambola.

“Do you truts her? Aliuliza Thomas

“Yes I do” alijibu Ambola.

“Thomas endelea tafadhali” alisema Gosu Gosu.

“Mimi ni jasusi wa Congo nchini Tanzania.Nimewekwa hapa makusudi kabisa kwa ajili ya kufanya kazi ya kulinda usalama wa Congo.Kazi hii ndiyo iliyonikutanisha na Julius Kabembo baba yake Ambola tukawa marafiki.Julius alikuwa mfanyakazi wa siri wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi inajulikana kama SNSA.Alifahamu hatari iliyomkabili kuhusiana na hizo

ramani alizokueleza Ambola, akaniomba kama jambo lolote baya litamfika basi nihakikishe ninamlinda Ambola. Na ndivyo nilivyofanya.Ili Ambola awe salama nilifanya mpango akaingia katika kambi ya wakimbizi" alisema Thomas.Alimtazama Gosu Gosu ambaye macho yake yalionesha alikuwa na kiu ya kufahamu zaidi.

Thomas alimueleza Gosu Gosu kila kitu kilichotokea tangu Ambola alivyofika katika kambi ya wakimbizi

alivyotolewa na kukutanishwa na familia ya Bernadetha hadi alivyopelekwa nje kupata mafunzo.Alimueleza pia kuhusu mahusiano ya Ambola na mzee Perfect.Sura ya Gosu Gosu ilibadlika.

“Ulikuwa na mahusiano na baba yako? Aling’aka Gosu Gosu

“Tuweke kumbukumbu vyema.Yule si baba yangu kama alivyosema Thomas.Ni mtu ambaye nilipelekwa kwake anilee.” Alisema Ambola.

“Pamoja na hayo hukupaswa kuingia katika mahusiano na mzee yule ambaye kila mtu hapa mjini anafahamu ni baba yako” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu, Ambola kuwa na mahusiano na mzee Perfect ni mpango maalum tulioupanga” Alisema Thomas na kumuelezea Gosu Gosu kile ambacho Ambola alikipata kutoka kwa mzee Perfect ukiwamo mpango wa kumuua.

“Baada ya Ambola kuunasa mpango huo, alikuja

kwangu akanieleza na kuniomba nimsaidie kufanya kila linalowezekana kukuokoa” Thomas alimweleza Gosu Gosu kile walichokifanya hadi walipofika mahali alipokuwa na wakafanikiwa kumuokoa.

“Kwa hiyo Gosu Gosu huo ndio mchezo mzima ulivyokuwa.Ni misheni iliyochukua muda mrefu sana kuiandaa na sasa umefika wakati wake.Ambola anahitaji msaada wako.Anahitaji kuonana na Mathew Mulumbi.” Alisema

Thomas.Gosu Gosu alimtazama Ambola kwa makini halafu akacheka kidogo.

“Unataka kuonana na Mathew Mulumbi” alisema Gosu Gosu.

“Ndiyo nahitaji kuonana na Mathew Mulumbi.Lengo kuu la kukuokoa ni ili unikutanishe na Mathew Mulumbi” alisema Ambola.

“Unadhani baada ya haya yote yaliyotokea nitakuamini tena? Ninafahamu ujanja wenu.Mmeamua kutumia njia

hii ili niwaamini na niwakutanishe na Mathew Mulumbi.That'll never happen" alisema Gosu Gosu.

"Gosu Gosu ninachokwambia ni kitu cha kweli.Hiki ni kikundi cha watu wenye mipango miovu sana kwa nchi yetu.Hawalali.Wanakesha kuhakikisha mipango yao inatimia." Alisema Ambola.Gosu Gosu alitafakari kwa muda halafu akasema

"Ukitaka niamini kama haya yote uliyonieleza ni

mambo ya kweli nataka nizipate ramani hizo ambazo umesema ndizo chanzo cha wewe kupitia haya yote uliyopitia.” Alisema Gosu Gosu.Ambola alimtazama Thomas.

“Sina tatizo na kukuonesha ramani hizo mradi tu uniahidi kuwa utanikutanisha na Mathew Mulumbi” alisema Ambola.

“Nikijiridhisha kuwa ramani hizo zina maana nitakukutanisha na Mathew Mulumbi” alisema Gosu Gosu.

“Thomas nipeleke nikamuoneshe Gosu Gosu ramani zile” alisema Ambola

“Una hakika Ambola unataka kumonesha ramani zile? Thomas aliuliza.

“Ndiyo.Nina uhakika” alijibu Ambola.Thomas alikwenda chumbani kwake akachukua bastola nyiungine yenye kiwambo cha sauti akampatia Gosu Gosu.

“Ya nini hii? Aliuliza Gosu Gosu.

“Kujihami.Hakuna anayejua nini kinaweza kutokea njiani” alisema Thomas.

“Ule msalaba unao? Aliuliza Thomas kabla hawajatoka mle ndani.

“Ndiyo ninao” alijibu Ambola.

Waliingia katika gari la Thomas wakaondoka kuelekea katika nyumba ambako Julius Kabembo alizihifadhi ramani.

****

“Ni miaka zaidi ya kumi tangu nilipofika katika nyumba hii” aliwaza Ambola baada ya kulikaribia geti la nyumba wanayokwenda.Taa za nje zilikuwa zinawaka kana kwamba kuna mtu anaishi.Thomas aliwataka wengine wote wabaki garini, akashuka akaelekea katika nyumba iliyojengwa kandoni mwa nyumba ile.Aligonga mlango na sauti kutoka ndani ilitaka kufahamu ni nani anayegonga.Thomas

alijitambulisha na baada ya dakika chache mlango ulifunguliwa jamaa mmoja akatoka.Alizungumza kidogo na Thomas halafu akarejea ndani akatoka na kitanza mbali akalifungua geti.Gari la akina Thomas liliingia ndani yule jamaa akabaki nje.

Watu wote walishuka garini.Thomas akamuomba Ambola ampatie ule msalaba.Aliuvuta kwa nguvu akang'oa kifuniko upande wa chini na wote walibaki na mshangao.Ilikuwa ni diski

mweko.Thomas aliusogelea mlango akaichomeka ile diski mweko katika tundu lililokuwa mlangoni.Alisubiri kwa sekunde kadhaa pale mlangoni na mara wote walishuhudia taa zikiwaka ndani.

“Teknolojia ya hali ya juu sana hii” alisema Jackline kwa sauti ndogo.Sauti za vyuma vikiachia mlangoni ilisikika halafu mlango ukafunguka.Waliingia ndani.Ambola machozi yalimtoka alipoinga tena ndani ya nyumba ile.

“Nini kinakuliza? Aliuliza Gosu Gosu.

“Ni miaka zaidi ya kumi imepita tangu nilipokuja na baba katika nyumba hii.Ilikuwa ni siku ya mwisho kufurahi na baba yangu” Alijibu Ambola.

“Pole Ambola” alisema Jackline.Gosu Gosu alimtazama hakusema chochote.

Thomas ambaye alionekana kuifahamu vyema nyumba ile aliwataka wamfuate.Walifika katika

chumba ambamo zilihifadhiwa zile ramani.Aliichomeka diski katika mlango na kusimama akisubiri hadi pale kitasa kilipoachia akaufungua mlango wakaingia ndani.Kila kitu kilikuwa vile vile kama kilivyokuwa siku ile alipokuja na baba yake.

“Ambola unazikumbuka namba za kufungulia kasiki? Aliuliza Thomas.

“Ninazikumbuka” alijibu Ambola.

Alilisogelea kasiki akaingiza namba zile

alizopewa na baba yake ambazo hazikuwahi kumtoka kichwani, kasiki likafunguka.Huku mwili ukimtetemeka aliingiza mkono ndani ya kasiki akatoa karatasi tatu zilizokunjwa vizuri.Alimkabidhi Thomas karatasi zile.Aliikunjua ya kwanza ilikuwa ni ramani ya Tanzania.Aliitazama halafu akamkabidhi Gosu Gosu.Aliitazama akaiweka pembeni akaichukua ramani ya Afrika akaitazama akaiweka pembeni halafu akaichukua

ramani ya dunia akaitazama na kuiweka pembeni.

Ndani ya kasiki lile walikuta pia kuna diski mweko.Ambola aliichukua na kumpatia Gosu Gosu.

“Naamini ndani ya diski hii kuna mambo ya muhimu ndiyo maana baba aliihifadhi humu” alisema Ambola.Gosu Gosu aliichukua diksi ile akaiweka mfukoni kisha wakatazamana.

“Unaniamini sasa? Aliuliza Ambola.Wote waliyaelekeza

macho yao kwa Gosu Gosu kusubiri jibu lake.

“Kidogo ninashawishika japo bado sina imani nawe tena, ila nitakufikisha kwa Mathew Mulumbi.Lakini ni wewe pekee” alisema Gosu Gosu.

“Hapana.Tunakwenda sote.Sisi ni timu moja.” Alisisitiza Ambola.

“Gosu Gosu huna haja ya kuhofu.Muamini Ambola” alisema Thomas.Gosu Gosu alifikiri kidogo halafu akasema.

“Naomba simu”

“Jackline mpe simu yako” alisema Ambola.Jackline alimpatia Gosu Gosu simu yake akatoka ndani ya kile chumba.

****

Ukimya wa Mathew Mulumbi ulimuogopesha Ruby.

“Mathew naomba tafadhali utueleze ni nani huyu Israel Maungwana? Aliuliza Ruby.

Bado Mathew aliendelea kuitizama picha ya Israel

katika runinga.Simu ya Ruby iliita.Aliichukua akaitazama.Ilikuwa ni namba ngeni isiyo na jina, akaipokea.

“Halloo” alisema Ruby

“Ruby ni mimi Gosu Gosu”

“Gosu Gosu ! Rby alishituka.Mathew naye aliposikia Ruby akilitaja jina la Gosu Gosu alishituka akageuza shingo kumtazama.

“Uko wapi Gosu Gosu? Aliuliza Ruby

“Kwa sasa niko huru.Niko Dar es salaam”

“Uko Dar es salaam? Aliuliza Ruby.

“Ndiyo.Ruby nahitaji kuzungumza na Mathew.Uko naye karibu?” aliuliza Gosu Gosu.Haraka haraka Ruby alimpatia Mathew simu.

“Gosu Gosu” alisema Mathew

“Mathew nimefurahi kukusikia tena.Mimi niko salama nimefanikiwa kutoka katika mikono ya wale watu washenzi.Tayari niko Dar es salaam.” alisema Gosu Gosu.

“Good.Uko wapi sasa hivi? Aliuliza Mathew

“Ninahitaji kujua mahali mlipo ili niwafuate.Nitawaeleza kila kitu nitakapofika” alisema Gosu Gosu.Mathew alimuelekeza mahali walipo na kukata simu.

“Mathew unamuamini Gosu Gosu? Hudhani ametumiwa na watu wanaomshikilia ili kufahamu mahali ulipo?” aliuliza Ruby.

“Ninamuamini Gosu Gosu.Hawezi kutuuza.Yuko

tayari kuutoa uhai wake kuliko kuwasaliti ndugu zake” alisema Mathew ambaye hakuonesha hata chembe ya wasi wasi.

“Mathew huwezi kujua yawezekana amepewa mateso makali akashindwa kuvumilia akaamua kuonesha mahali tulipo” alisema Ruby

“Nimekuwa na Gosu Gosu kwa kipindi kirefu ninamfahamu vyema.Si mtu ambaye anaweza akafunguka kirahisi.Ana uwezo mkubwa sana wa kuvumilia mateso ya

aina yoyote.Kamwe hawezi akasaliti wenzake” alisema Mathew.

“Sawa.Wakati tunamsubiri Gosu Gosu turejee katika lile suala letu la awali.Tuliishia kwa mwenyekiti wa chama cha kombozi wa Afrika ndugu Israel Maungwana.Ni nani huyu mtu? Aliuliza Ruby.

“Naomba tuliweke kwanza pembeni jambo hili.Tuna mengi ya kufahamu kutoka kwa Gosu Gosu.Tunaweza kupata mambo ambayo yanaweza kutusaidia sana

katika jambo hili.” alisema Mathew akamgeukia Regina.

“Ulikuwa umeanza kutueleza kuhusu mwenyekiti wa chama chako Israel Maungwana.Endelea tafadhali”

“Kama nilivyowaambia, sina mahusiano ya karibu sana na mwenyekiti. Hatukuwa na mahusiano nje ya yale ya kikazi hivyo siwezi kumuelezea vizuri ni mtu wa aina gani” alisema Regina.

“Yule jamaa si mtu anayependa kutengeneza marafiki” aliwaza Mathew.

“Vipi kuhusu familia yake? Aliuliza Ruby

“Mke wake ni mzungu.Nimewahi kumuona mara mbili.Alifika pale makao makuu kumfuata mume wake” alisema Regina na mara Mathew akashituka.

“Ruby tafuta mtu anaitwa Diana Watvon”alisema Mathew.Bila kuhoji chochote Ruby akitumia mfumo wa SNSA alifanikiwa kumpata

mtu yule.Picha ya mwanamke wa kizungu ilionekana katika runinga kubwa.

“That’s her.Yule ndiye mke wa Israel” alisema Regina.

“Mathew inaonekana unamfahamu sana huyu mtu.Unaweza ukatueleza huyu mtu ni nani? Aliuliza Ruby.

Ilimchukua Mathew dakika mbili za ukimya halafu akasema.

“Jina lake si Israel Maungwana.Jina lake halisi ni Hammar Perezi.Israel

Maungwana ni jina bandia kwa sababu anazozijua yeye na hata ukichunguza kwa undani sana utagundua hakuna ukweli kuhusu jina hilo.Nilifanya naye kazi katika shirika la ujasusi nikiwa katika kitengo cha kudhibiti ugaidi.Hatujui alitoka wapi lakini tulianza kumuona katika ofisi zetu bila kufahamu kazi yake.Mkurugenzi wa shirika, alikuwa rafiki yangu mkubwa ndiye aliyenipa siri ya huyu mtu.Aliniambia jina lake halisi ni nani lakini hata yeye mwenyewe hakuwa na uhakika

na uraia wa huyu mtu.Hakujua kama yule jamaa ni mtanzania au anatokea taifa gani.Aliniambia kuwa alipewa maelekezo ya kuanzisha idara maalum ya siri kwa ajili ya kutekeleza shughuli maalum" alinyamaza kidogo.

"Nani alimpa maelekezo hayo? Aliuliza Ruby.

"Hakumtaja jina aliyempa maelekezo hayo lakini alisema ni kutoka ngazi za juu.Hammar ndiye aliyeletwa kuja kuongoza idara hiyo ya siri ndani ya shirika.Idara hiyo

ilikuwa ni kwa ajili ya kufanya kazi mbali mbali za wakubwa na hasa mauaji.Kupitia idara hiyo mauaji mengi ya viongozi yalifanyika hasa wale waliokuwa na mlengo tofauti na serikali, wakosoaji wa serikali, wapinzani na yeyote ambaye alionekana ni hatari kwa nchi aliondolewa uhai.Kwa ufupi ninaweza kusema kuwa kitengo kile kilikuwa ni kitengo cha mauaji.Jina lako likipelekwa ndani ya kitengo hicho hakuna mahali unakoweza kukimbilia duniani kukwepa mkono

wao.Walikuwa na uwezo mkubwa wa kupenya na kuingia katika nchi yeyote wakafanya mauaji.” Alinyamaza tena kidogo.

“Tulipata taarifa za siri kuwa mwanamke mmoja gaidi kutoka nchi moja ya kiarabu aliingia hapa nchini.Tulianza kumfuatilia mwanamke huyo tukagundua hakuwa peke yake.Alikuwa ameongozana na mwanamke mwingine anaitwa Diana Watvon.Huyu Diana Watvon ni mwanamke shetani.Anatumiwa na

mabeberu katika mipango yao miovu dhidi ya bara letu la Afrika.Huyu ni bingwa wa kutengeneza migogoro.Karibu migogoro mingi ambayo imetokea barani Afrika na kusababisha umwagikaji mkubwa wa damu ukichunguza kwa undani sana utakuta kuna mkono wa huyu mama.Anatengeneza migogoro ya nchi kwa nchi, jamii kwa jamii na kusababisha machafuko na umwagikaji wa damu.Mwanamke huyo licha ya kuwa ni bingwa wa kutengeneza migogoro vile vile

ni jasusi.Umuonapo mahali lazima kuna kitu anakitafuta.Amekuwa pia ni kiunganishi kati ya mataifa makubwa na mitandao ya kigaidi.Kuna tetesi kuwa mataifa haya makubwa wamekuwa wakiyatumia makundi ya kigaidi ili kufanya mashambulio sehemu mbali mbali duniani kwa maslahi yao, hizi si tetesi ni kitu cha kweli kabisa.Huyu mama ndiye wakala.Anawafahamu magaidi wote na namna ya kuwafikia.Nilimuita shetani si kwa kumvua utu bali ni kwa

unyama wake.Ni mwanamke katili sana.” Alisema Mathew na kuitazama tena picha ile ya Diana katika runinga.

“Ilikuaje hadi akaolewa na Israel? Aliuliza Regina.

“Nitawarudisha nyuma kidogo.Baada ya kupata taarifa zile za yule mwanamama gaidi na kumfuatilia tuligundua alikuwa na mpango wa kukutana na watu kadhaa kwa lengo la kuanzisha kikundi cha ugaidi hapa nchini.Nikiwa kama mkuu wa kitengo cha kudhibiti ugaidi nilitoa

mapendekezo ya kumkamata yule mwanamke ili tufahamu watu anaoshirikiana nao.Tulijiandaa na kuingia katika misheni hiyo lakini tulipofika eneo la tukio badala ya kufanikisha misheni yetu tulijikuta tukipambana na kikundi cha watu waliojihami vyema kwa silaha nzito.Ilikuwa ni kama vita ndogo.Watu wote niliokuwa nao waliuawa.Nilibaki peke yangu nikakimbia.Nilielekea nyumbani kwangu ambako nilikutana na kitu cha kusikitisha.Nyumba yangu

ilikuwa inateketea moto huku familia yangu ikiwa ndani.Nilichanganyikiwa.Niki wa eneo la tukio nilifuatwa kwa lengo la kuniua.Ni mkurugenzi aliyeniokoa kwa kunitumia mtu aliyenitoa eneo la tukio. Huo ulikuwa mwisho wangu kufanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania. Nilikimbilia nje ya nchi kwa ajili ya usalama wangu. Nikiwa huko mkurugenzi alinijulisha kuwa shambulio lile lilifanywa na Hammar na idara yake ya siri.Niliambiwa kwamba baada ya kutokea tukio lile,

uchunguzi ulifanywa na ilibainika kuwa Hammar alikuwa na mawasiliano na Diana Watvon.Baada ya hapo Hammar alitoweka kimya kimya na ukawa mwisho wa idara ile ya siri ya mauaji. Nimeshituka kumuona tena akiwa ndiye mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika.Kibaya zaidi ameficha jina lake na anatumia jina bandia la Israel Maungwana.Huyu jamaa ni kibaraka.Ni mtu wa kutumiwa na mabeberu. Uwepo wake katika siasa za upinzani hapa

Tanzania unazidi kuthibitisha kuwa upo mpango mbaya dhidi ya uchaguzi wetu.” Alisema Mathew.

“Ahsante Mathew kwa maelezo hayo ambayo yametupa picha pana kabisa kuhusiana na huyu mtu na kile tunachokichunguza” alisema Ruby

“Kitu kingine ambacho lazima mfahamu, Hammar na Diana si mke na mume.Hawa ni washirika.Mashirikiano yao hayajaanza leo. Nadhani wote wako hapa kwa ajili ya

kutekeleza mpango huo wa kuhujumu uchaguzi mkuu” Mathew aliongeza.

“Nini kinafuata Mathew? Tunasubiri mwongozo wako.” Alisema Ruby.

“Gosu Gosu amesema anakuja na jambo zito.Tumsubiri tujue ana jambo gani la kutuambia.Ni yeye aliyetumiwa katika mpango wa kumuua Regina.Tunahitaji kujua je wale waliomtuma kumuua Regina wana mahusiano yoyote na chama cha siasa cha

Ukombozi wa Afrika ambacho Israel ndiye kiongozi wake? Regina anahisi chama chake ndio wanaotaka kumuua lakini hatuna uhakika bado kama kweli ni wao hivyo maelezo ya Gosu Gosu yatatupa picha tutajua ni wapi tuelekee" alisema Mathew na kuinuka akaelekea chumbani kwake.

"Mathew amekumbushwa mbali sana baada ya kumuona Israel.Sijawahi kumuona akipatwa na hofu kiasi hiki.Amekumbushwa kuhusu

familia yake iliyoteketea” alisema Ruby

“Hata mimi maelezo yake yamenifanya nikaogopa sana.Sikujua kama Israel ni mkatili kiasi hicho.Kumbe niliyaweka maisha yangu hatarini pale nilipoanza kufukunyua siri za chama.Nimeogopa sana” alisema Regina.

****

Kupitia kamera ya getini, Ruby aliziona gari mbili zikilisogelea geti la nyumba waliyokuwamo.Alimfuata Mathew chumbani kwake akamkuta akiwa amekaa kitandani ameinamisha kichwa.

“Mathew gari mbili zinakaribia geti.Nahisi ni Gosu Gosu” alisema Ruby.

“Kwa nini gari mbili? Ina maana Gosu Gosu hayuko peke yake” alisema Mathew huku akinyanyuka na

kuongozana na Ruby kuelekea katika ofisi yao.Gari zile mbili zilifika getini na mara simu ya Ruby ikaita.

“Ni Gosu Gosu.Hizi ndizo namba alizotumia kunipigia wakati ule.” Alisema Ruby akaipokea ile simu.Ni kweli, Gosu Gosu ndiye aliyepiga simu.Alimjulisha Ruby kuwa tayari amefika.Mathew alitoka akaelekea getini akalifungua gari zile mbili zikaingia ndani. Gosu Gosu ndiye aliyekuwa wa kwanza

kushuka.Alimkumbatia Mathew kwa furaha kubwa.

“Karibu tena Gosu Gosu.Pole sana kwa yote uliyopitia” alisema Mathew.

“Mathew ninamshukuru sana Mungu kwa kunitoa katika mikono ya wale mazimwi watu” alisema Gosu Gosu.

“Hallow Mathew” sauti ya Ambola ilisikika kutoka nyuma yake.

“Ambola” alisema Mathew kwa mshangao.Hakutegemea

kumuona Ambola mahali pale.Walikumbatiana kwa furaha.

“Karibu sana Ambola.Nimefurahi kukuona tena.” Alisema Mathew akamgeukia Gosu Gosu.

“Gosu Gosu kwa nini hukunijulisha kama unakuja na wageni?

“Samahani sana Mathew kwa kutokujulisha kama nitakuja na watu wengine” alisema Gosu Gosu.

“Hakuna tatizo .Usingewaleta hapa kama hawana umuhimu kwetu.Kikubwa ninachotaka unihakikishie kama hakuna mkia uliowafuata” alisema Mathew.

“Tuko salama kabisa hakuna mkia uliotufuata”

“Good.Karibuni ndani” alisema Mathew.Aliwaongoza wageni wakaingia sebuleni.Gosu Gosu alikumbatiana na Ruby kwa furaha kubwa.

“Wageni wetu karibuni sana.Mimi naitwa Mathew Mulumbi.Mwenzangu anaitwa Ruby” Mathew alianza utambulisho.

“Mimi na Ambola mnatufahamu.Tulioongozana nao ni….” Alisema Gosu Gosu na kuwageukia akina Thomas.

“Thomas Ngalula” alisema Thomas.

“Naitwa Jackline Mo.” Alisema Jackline.

“Karibuni sana jamani’ alisema Mathew.

“Tunashukuru sana” walijibu akina Thomas.

“Kuna yeyote anahitaji kinywaji? Bia, maji” alisema Ruby.

“Ahsante Ruby.Kwa sasa ni muda wa kazi” alisema Gosu Gosu.

“Mathew kama ulivyosema wewe mwenyewe kuwa watu hawa ni muhimu sana kwetu ndiyo maana niko nao hapa.” Alianza Gosu Gosu.

“Mimi na Ambola tumekuwa ni wapenzi kama

ufahamuvyo lakini siku chache zilizopita kuna jambo lilitokea nika….” Alisema Gosu Gosu, Mathew akamkatisha.

“Ruby hebu muite Regina’ alisema Mathew na Regina akaitwa.

“Regina nimekuita hapa kwa sababu mazungumzo haya nawe yanakuhusu” alisema Mathew na Regina akaketi.Gosu Gosu akaendelea.

“Lilitokea jambo katika siku ya kuzaliwa Ambola.Sitaki kulielezea hapa kwa sababu tayari nyote mnalifahamu.”

Alisema Gosu Gosu.Mathew na Ruby wakatazamana.

“Gosu Gosu kuna watu hapa ambao hawafahamu nini hasa kilichotokea.Wafahamishe nini kilichotokea.Tunataka kila mmoja hapa afahamu kilichotokea na kile kinachoendelea ili wote tusome ukurasa mmoja” alisema Mathew.Gosu Gosu alieleza kila kitu kilichotokea katika sherehe ile ya kumbukumbu ya kuzaliwa Ambola.Kilichowashangaza

Mathew na Ruby, Ambola hakuonesha mshituko wowote kwa maelezo yale. Gosu Gosu aliendelea kueleza kilichofuata baada ya tukio lile.

“Sikuweza kukataa nilipotakiwa kwenda Arusha kufanya mauaji kwa sababu sikutaka Ambola afahamu kile kilichokuwa kimetokea.” Alisema Gosu Gosu na kuendelea kueleza kilichotokea Arusha hadi tukio la mwisho lililotokea Duma Bar.

“Sikumuua Regina kama nilivyotakiwa na kwa kitendo

hicho niliharibu kazi ya watu waliyonituma” alisema Gosu Gosu.Regina aliyekuwa anasikiliza kwa makini alifuta machozi.

Gosu Gosu aliendelea kueleza kilichomtokea baada ya kushindwa kumuua Regina hadi alivyokombolewa na Thomas kisha akapelekwa kuonana na Ambola.

“Kwa hiyo Bernadetha ameuawa” alisema Mathew.

“Ndiyo ameuawa.” Alijibu Gosu Gosu.

“Dah !” alisema Ruby.

“Baada ya kuonana na Ambola ndipo nilipofumbuka macho zaidi kwa mambo mazito niliyoyafahamu kutoka kwake.Ambola uwanja ni wako, eleza kile kilichotokea” alisema Gosu Gosu.

Ambola alianza kumweleza Mathew historia yake hadi tukio lililomtokea baba yake na hadi alivyopelekwa katika kambi ya wakimbizi Kasulu Kigoma.Alimpa pia nafasi Thomas aliyeeleza namna

alivyoweza kumuingiza Ambola katika mtandao wa akina Bernadetha huku wakifahamu kuwa ni raia wa Congo.Kila kitu kiliwekwa wazi hadi Ambola alivyofanikiwa kupata siri kutoka kwa Perfect kuhusu mpango wa kuhakikisha wanakiondoa madarakani chama kinachotawala vile vile mpango wa kumuua Gosu Gosu.

“Baada ya kufahamu kuhusu mpango huo wa kumuua Gosu Gosu nilimfuata

Thomas nikamtaka anisaidie kumuokoa kwani ni yeye anayefahamu mahali ulipo.” Alisema Ambola.

“Hili ni jambo zito sikulitegemea kabisa.Kwanza ninakupa pole kwa yote uliyopitia.Si mambo rahisi lakini umevumilia hadi ukafika hatua hii.Ulivaa vyema uhusika wa kuwa raia wa nchi nyingine kiasi kwamba hakuna mtu aliyewahi kukutilia shaka kuwa wewe si raia wa Congo.Pili ninakupongeza kwa kazi kubwa uliyoifanya hadi

ukaweza kugundua kuhusu mpango wa kumuua Gosu Gosu na ukishirikiana na Thomas mkafanikiwa kumuokoa.Ahsante sana Ambola na wote mlioshiriki katika mpango huu" alisema Mathew.

"Imekuwa vyema tumesikia maelezo yenu ambayo tukiyaunganisha na kile tunachoendelea kukifanya tunapata picha kubwa ambayo itatusaidia sana katika uchunguzi wetu.Labda niwape picha kidogo ya kile ambacho

tunakishughulikia sasa hivi.Baada ya kumuokoa Regina tulimuhoji sababu ya yeye kutaka kuuawa na jibu alilotupa ni kuwa anatakiwa kuuawa baada ya kuzifahamu siri kadhaa za chama chake cha Ukombozi wa Afrika.Kwa msiomfahamu, Regina alikuwa naibu katibu mkuu wa chama hicho.Mojawapo ya siri aliyoifahamu katika chama hicho na ambayo anaamini ni sababu ya yeye kutakiwa kuuawa ni kugundua uwepo wa njama za kuvuruga uchaguzi mkuu wa Rais na

wabunge.Regina alipewa siri ya uwepo wa njama hizo ovu na dereva wa mwenyekiti ambaye aliuawa na Gosu Gosu.Siku aliyouawa ni siku ambayo alikuwa amepanga kumpatia Regina taarifa ya uchunguzi wote alioufanya kuhusiana na mipango ya mwenyekiti na chama chao lakini kwa bahati mbaya alikufa kabla hajawasilisha taarifa yake.Hatujui ni namna gani watu hao wamepanga kuhujumu uchaguzi mkuu.” Alisema Mathew

“Laiti ningejua yule jamaa alikuwa na taarifa muhimu nisingemuua” Gosu Gosu alijilaumu.

“Hupaswi kujilaumu.Hakuna aliyefahamu jambo hilo” alisema Mathew.

“Kwa maelezo ya Ambola tumeanza kupata picha namna wanavyotaka kuhujumu uchaguzi mkuu. Wanataka kukiondoa madarakani chama kinachotawala na kukiweka madarakni chama kingine wanachokitaka wao.Maneno

haya yanaashiria wazi kuwa watu hawa ni mtandao mkubwa unaohusisha watu wengi.Kauli hii inaonesha wazi kuwa hawa ni watu wenye maamuzi ya nini kifanyike nchini.They’re powerful people.Si watu wa kufanyia mzaha hata kidogo.Tumesikia maelezo ya Thomas kuwa jambo hili halijaanza leo.Wameanza kulianda zaidi ya miaka kumi iliyopita.Lazima kuna hatua kubwa wameipiga hadi sasa ndiyo maana wanajiamini sana

kuwa lazima mipango yao itafanikiwa.” Alisema Mathew.

“Mathew, huu mtandao unapewa nguvu na watu kutoka mataifa ya nje. Hawa watu ambao ninyi mnawaita mabeberu mpango wao ni kuishika sehemu kubwa ya Afrika.Wanazilenga nchi kumi kwa kuanzia na kisha wataendelea kujipenyeza taratibu katika nchi nyingine.Hawajishughulishi na nchi ambazo hazina manufaa kwao.Wanazilenga nchi zile zenye rasilimali nyingi.Kama

nilivyoeleza kuwa mpango wa Congo mpya unategemea sana kufanikiwa kwa mpango wa Tanzania mpya ambao ni kukiondoa madarakni chama kinachotawala na kukiweka chama wanachokitaka wao ambacho ni ukombozi wa Afrika.Tukifanikiwa kuzima mpango wa Tanzania mpya na kuufagia mtandao wao basi hakutakuwa na mpango wa Congo mpya ndiyo maana niliamua kumuua Joseph Tshibanga. Gosu Gosu alinilaumu lakini kazi yangu ni kuhakikisha nchi yangu

inakuwa salama ndiyo maana nimejipachika katika mtandao huu bila kujulikana” alisema Thomas.

“Mathew kuna jambo ambalo nataka kuliweka wazi nalo ni kushiriki katika mtandao wa Congo mpya. Nilishirikishwa katika mpango huo na Joseph Tshibanga.Huyu alikuwa rafiki yangu.Tulikutana msituni katika kikundi cha waasi tukipambana na serikali.Mwenzangu alikuwa tayari na elimu hivyo hakukaa

sana aliondoka msituni na tulikuja kukutana tena hapa Tanzania siku alipokuja Rais wa Congo na kufanya mkutano na wacongo wote waishi hapa Tanzania. Tulipokutana alinifahamisha uwepo wa mpango wa Congo mpya akanishawishi nikajiunga katika mtandao wao.Sikujua kumbe tulikuwa na mashirikiano na akina Bernadetha" alisema Gosu Gosu.

"Gosu Gosu tutayazungumza hayo

baadaye.Kwa sasa tujielekeze katika mambo muhimu yaliyoko mezani. Nataka kufahamu ni namna gani wanataka kuitumia Tanzania katika mpango wa Congo mpya? Aliuliza Mathew

“Mpango uliopo ni huu.Baada ya kukiondoa madarakani chama kinachotawala na kukiweka madarakani chama kingine, miongoni mwa viongozi watakaoalikwa kuhudhuria sherehe za kuapishwa rais mpya ni Jenerali Salvatory

Mamba. Atakapokuja Tanzania hataondoka salama.Umetengenezwa mpango kabambe wa kumuua” alisema Thomas.

“Mpango huo wa mauaji umeandaliwaje? Aliuliza Mathew.

“Bado ni siri.Mpango wa mauaji ya Jenerali Mamba unafanywa kwa siri kubwa.” Alijibu Thomas.

“Kabla hamjafika hapa swali tulilokuwa tunajiuliza ni je Bernadetha na genge lake wana mahusiano yoyote na

chama cha ukombozi wa Afrika? Kwa maelezo tuliyoyapata kutoka kwa Ambola inaonesha wazi watu hawa wana mashirikiano lakini lazima tujiridhishe je tunashughulika na makundi mawili au ni kundi moja?.Ninachowaomba sote tuunganishe nguvu kwa kuwa nia yetu ni moja.Kama mko tayari kwa hilo basi Ambola utafanya kazi hiyo ya kumchunguza Perfect ili tujue kama ana mashirikiano na viongozi wa chama cha ukombozi wa Afrika. Tayari

umemuweka kiganjani hivyo itakuwa rahisi kuchota siri mbali mbali kutka kwake japo umakini mkubwa sana unatakiwa” Alisema Mathew.

“Nitaifanya kazi hiyo.Hata hivyo kuna jambo lingine ambalo nilisahau kuwaeleza.Perfect alipigiwa simu na mke wake jana usiku akamtaka akawapokee wageni uwanja wa ndege.Alimpa majina ya wageni hao na namba ya ndege watakayopanda.Nilifanikiwa kunakili majina ya watu hao”

alisema Ambola na kumpatia Mathew kijikaratasi ambacho aliandika majina ya wale wageni waliowasili usiku.Mathew aliyapitia halafu akampatia Ruby.

“Hawa jamaa ni mtandao mkubwa na wanao watu wengi ambao wangeweza kuwatuma kwenda kuwapokea wageni hao lakini hawakufanya hivyo badala yake akaenda mzee Perfect mwenyewe kuwapokea.Hii inatoa picha kuwa wageni hao wana umuhimu mkubwa sana

kwao.Swali ni je wageni hao wana mahusiano yoyote na mipango hiyo ya kuhujumu uchaguzi mkuu? Aliuliza Mathew.

“Tunatakiwa kwanza kuwachuguza watu hawa ni akina nani na kisha tutachunguza mahusiano yao na akina Perfect.Tutapata jibu” alisema Ruby.

"Mathew pamoja na suala hili la hujuma lakini kuna jambo lingine ambalo ninataka kukushirikisha ambalo ni hili la hizi ramani.Maelekezo ya

baba yangu alipokuwa ananikabidhi ramani hizi ni kuhakikisha ninaziweka wazi kwa watanzania wafahamu kuhusu utajiri huu mkubwa uliofichwa katika sehemu mbali mbali za nchi yetu.Siwezi kuifanya kazi hiyo peke yangu ninahitaji msaada wenu.Tushirikiane kuhakikisha tunalifanikisha jambo hili.” Alisema Ambola.

“Ambola narudia kukupa pole kwa kumpoteza baba yako.Ninamsifu sana kwa uzalendo wake.Alikuwa tayari

uhai umtoke lakini asiinue mikono na kuonesha mahali zilipo ramani hizi muhimu sana.Huu ni ushahidi mkubwa wa namna gani nchi yetu na bara zima la Afrika linavyohujumiwa rasilimali zake.Kwa kuwa mabeberu hao wameendelea sana katika teknolojia, wamefanikiwa kufahamu kila sehemu yenye madini katika nchi hii lakini hawataki watanzania wafahamu ndiyo sababu ya ramani hii kufichwa.Wanataka kushirikiana na watanzania wachache waliokosa uzalendo

kwa nchi yao ili wanufaike na madini hayo.Hii ni sababu nikisikia neno beberu mwili wote unasisimka.Ninawachukia mabeberu kupita kiasi.Ambola usiwe na shaka tutalishughulikia suala hili na haki itapatikana kwa wale wote waliomuua baba yako.Lazima wote watafahamika.Kwa sasa ninaomba tujielekeze kwanza katika hili suala la kuhujumu uchaguzi mkuu.Nina uhakika mkubwa kwa kumchunguza Perfect tutaweza kufahamu kile kinachoendelea kuhusiana

na mipango hii ya hujuma.Ruby atakuwekea program Fulani katika simu yako ambayo utaiwasha pindi utakapokuwa karibu na simu ya Perfect.Programu hiyo itaiunganisha simu ya Perfect na kompyuta yetu hivyo tutaweza kufuatilia mawasiliano yake.Jambo la pili, kufuatia kifo cha Bernadetha itakubidi uhudhurie msibani.Ukiwa pale msibani utaendelea kufanya uchunguzi wa kila kinachoendelea.Kuna mtu ambaye ninataka umchunguze

kama atafika msibani” alisema Mathew akamgeukia Ruby akamtaka ampatie picha ya Israel Maungwana.

“Nataka ukiwa msibani uchunguze kama huyu mtu atafika msibani.Huyu anaitwa Israel Maungwana.Ni mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika.Kama atafika msibani basi moja kwa moja tutajua hawa watu wanashirikiana.Jambo lingine utavaa kamera maalum ambayo itatuwezesha sisi kufuatilia kila kinachoendelea

hapo msibani.” Alisema Mathew na kumgeukia Jackline.

“Dada ulisema unaitwa nani?

“Naitwa Jackline Mo.”

“Jackline Mo karibu sana.Ambola ametueleza kuwa wewe ni mlinzi wake.Kukubali kwake wewe ufike mahali hapa inaonesha imani kubwa aliyo nayo kwako.Kwa kuwa yeye amekuamini nasi pia tunakuamini.Nataka ujiunge katika harakati zetu za kupambana na wale

wanaohujumu rasilimali za nchi yetu wakishirikiana na mabeberu.Sisi ni wazalendo wachache ambao tuko tayari kuyaweka hatarini maisha yetu kwa ajili ya kuipigania nchi yetu.Hatulipwi na wala serikali haijui kama tunafanya misheni hii.Kazi hii ni ya kujitolea.Kama nawe ni mzalendo wa kweli ambaye una uchungu na nchi yako naomba ujiunge nasi ili tupambane tuhakikishe hakuna mpango wa mabeberu dhidi ya nchi yetu utakaofanikiwa. Umesikia yote

yaliyozungumzwa hapa ni mambo mazito sana. Naamini umepata picha pana ni namna gani nchi yetu inavyochezewa na watu wachache vibaraka wa mabeberu. Watu waliokupa kazi ya kumlinda Ambola ni watu wabaya sana ambao wana mipango mibaya sana dhidi ya nchi yetu. Kama nawe ni mmoja wa watu wenye uchungu na nchi yako unaweza ukajiunga nasi katika harakati hizi" alisema Mathew.

"Ninakushukuru sana kaka kwa kunikaribusha mahali

hapa na kuniruhusu nikashiriki katika majadiliano yenu.Kwa ufupi tu sikuwa nkifahamu chochote kinachoendelea hapa nchini. Ninaweza kusema ni Mungu aliyenikutanisha nanyi. Mimi ninatokea Arusha, nilipigiwa simu na rafiki yangu mmoja akaniomba nije Dar es salaam kuna kazi ya kufanya yenye hela nzuri.Nilikuja Dar na kupewa kazi ya kumlinda Ambola kuhakikisha anakuwa salama. Haya niliyoyasikia leo kuhusiana na kile kinachondelea katika nchi yetu

ni mambo yaliyonisisimua sana.Mimi ninatokea sehemu yenye madini ya pekee duniani na ninafahamu thamani ya madini tuliyonayo hivyo siko tayari kukubali hawa mabeberu wakafaidika na utajiri wetu.Nitashirikiana nanyi bega kwe bega kuhakikisha tunaharibu mipango yote ya mabeberu na vibaraka wao.Ninao uwezo mkubwa wa kuchezea silaha.Ninaweza kuendesha gari kwa umahiri mkubwa.Ninaweza kuwa

dereva wenu.” alisema Jackline.

“Ahsante sana Jackline kwa maneno yako mazuri.Ninawapenda watu kama ninyi.Pamoja na kukubali kwako kujiunga nasi naomba nikufahamishe kuwa kazi hii ni ya hatari mno.Watu hawa ambao tunapanga kuharibu mipango yao ni wazito.Nyuma yao kuna mabeberu wanaotoka nchi tajiri.Si mapambano rahisi.Hawataki kusikia msamiati wa kushindwa.Wao

wanachokihitaji ni mipango yao kufanikiwa.Kikwazo chochote kinachojitokeza ambacho kitakuwa hatari kwa mipango yao lazima wakiondoe mara moja.Tayari sisi ni kikwakzo kwao.Tumeifahamu mipango yao kitu ambacho hawakitaki hivyo hatutakuwa na maisha rahisi hata kidogo.Mfano mdogo tu ni Regina ambaye kwa sasa anatafutwa kwa kosa la mauaji.Tayari ameangushiwa mzigo wa yale mauaji ya Arusha na sasa anasakwa na jeshi la

polisi.Huu ni mfano mmoja kuonesha nguvu waliyo nayo hawa jamaa.Wanaweza wakatumia hadi dola.” Alisema Mathew.

“Umenikumbusha kitu Mathew.Wakati wananishikilia, Bernadetha aliwahi kuzungumza na kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha.Alimpa maelekezo ya kufuatilia katika ile hoteli uliyokuwa umefikia.” Alisema Gosu Gosu.

“Ahsante Gosu Gosu, sasa tumefahamu nguvu ya hawa

jamaa.Wanaweza wakatumia hata baadhi ya viongozi ndani ya jeshi la polisi katika kufanikisha mipango yao. Gosu Gosu lazima utahusishwa na mauaji ya Bernadetha.Maisha yetu hayatakuwa rahisi.Pamoja na ugumu huo tutakaokutana nao hakuna kukata tamaa.Tutapambana kuhakikisha mipango yao yote haifanikiwi.Nitatangulia mbele katika mapambano haya na kuhakikisha nyote mnakuwa salama.” Alisema Mathew na kuwaondoa hofu wenzake.

“Jackline utaongozana na Ambola msibani.Pamoja na kazi ya kuhakikisha anakuwa salama lakini vile vile nawe utakuwa na kazi ya kuchunguza kila kinachoendelea msibani hapo.Yawezekana kuna nyakati Ambola akashindwa kuwasiliana nasi au kuifanya kazi yake ya uchunguzi basi tutakutumia wewe.Utavaa miwani yenye kamera ambayo itatuwezesha kupata picha za kinachoendelea msibani.Sisi tutakuwepo karibu na mahali msiba utakuwepo.Tutakuwa

ndani ya gari maalum litakalokuwa limefungwa mitambo maalum ya kutuwezesha kuwasiliana nanyi .Nina uhakika mkubwa msibani hapo kuna jambo tutalipata litakalotusaidia katika uchunguzi wetu.Thomas wewe utaendelea na uchunguzi wako wa siri.Wachunguze viongozi wa vuguvugu la Congo mpya kuifahamu mipango yao hasa mpango wa kumuua rais wa Congo.Kikubwa ninachowasisitiza ni usiri.” Mathew alinyamaza baada ya

simu ya Ruby kuita.Alikuwa ni Faraji Dilele.Ruby alimtazama Mathew ambaye alimfanyia ishara kuwa aipokee ile simu.

“Hallow” alisema Ruby

“Ruby naomba kuzungumza na Mathew Mulumbi tafadhali” alisema Faraji.Ruby alimpa simu Mathew ili azugumze na Faraji.

“Hallow” alisema Mathew

“Mathew kuna taarifa yoyote mmeipata alfajiri hii?

Aliuliza Faraji, Sauti yake ilionesha wasi wasi mkubwa.

“Tangu tumerejea kutoka msituni hakuna taarifa yoyote tumeipata.Kuna taarifa gani? aliuliza Mathew.Faraji alivuta pumzi ndefu.Alionekana kutafuta aanzie wapi.

“Faraji kuna nini? Aliuliza Mathew.

“Nimepokea taarifa mbaya kuhusu Gavana”

“Kafanya nini Gavana? Aliuliza Mathew.

“Ametekwa na watu wasiojulikana alfajiri ya leo wakati akielekea kanisani.”alisema Faraji.Mathew alishituka na kuuliza.

“Ametekwaje ?

“Gavana ana kawaida ya kuhudhuria ibada kila siku alfajiri.Dakika chache baada ya kutoka nyumbani kwake zilitokea gari mbili na kulizuia gari lake.Walishuka watu wenye silaha na kuwapiga risasi dereva na walinzi watatu halafu wakamchukua

Gavana.Mpaka sasa haijulikani mahali alipo. Jeshi la polisi wanaendelea kumtafuta. Baada ya kupata taarifa hizo nimeona nikujulishe mara moja ili muwe makini.Hali ni mbaya” alisema Faraji.

“Ahsante sana Faraji kwa taarifa hii.Vipi kuhusu wewe unadhani utakuwa salama mahali ulipo? Aliuliza Mathew.

“Sifahamu Mathew lakini pale nitakapohisi hatari nitawajulisha mara moja” alisema Faraji na kuagana na Mathew.

“Kuna nini Mathew? Aliuliza Gosu Gosu.

“Gavana ametekwa nyara na watu wasiojulikana alfajiri ya leo.Hali inazidi kuwa mbaya” alisema Mathew.Kilipita kimya kifupi halafu akasema

“Ambola tayari kumepambazuka.Unatakiwa kurejea katika makazi yako.Unaweza ukatafutwa ukakosekana yakaibuka maswali mahali ulipo.” Alisema Mathew.Ruby aliichukua simu ya Ambola

akaiwekea ile program maalum halafu akampatia mkufu wenye kamera akamuelekeza namna ya kuutumia.Jackline Mo alipewa miwani myeusi yenye kamera.Wote walipewa vifaa vya kuweka sikioni kwa ajili ya mawasiliano kisha wakaondoka.

“Jamani, hamjalala usiku wa kuamkia leo lakini fahamuni hakutakuwa na hata dakika moja ya usingizi hadi pale tutakapohakikisha tumeiharibu mipango yote ya

mabeberu na kuwafagia vibaraka wao.Kutekwa kwa Gavana nina uhakika mkubwa kuna mahusiano na hiki kinachoendelea.Imeongezeka kazi nyingine ya kumtafuta na kuhakikisha anakuwa salama.Tuna mlima mrefu wa kupanda.” Alisema Mathew na kunyamaza baada ya simu ya Ruby kuita.

“Faraji anapiga tena” alisema Ruby na kumpatia Mathew simu akaipokea.

“Hallow” alisema Mathew.

“Mathew nimejulishwa kuna wa wamenifuata hapa nyumbani wanadai ni wanausalama wanahitaji nionane nao.Unanishauri nini? Nina hofu sana.”Aliuliza Faraji.

“Run !” Alisema Mathew

“Tafuta namna ya kutoka hapo nyumbani kwako bila kuonana nao. Kama nyumba yako ina mlango wa dharura, toka haraka kisha tujulishe. Hao siyo wanausalama. Tayari wamefahamu ulionana na

Gavana usiku wa kuamkia leo.” Alisema Mathew.

“Sawa Mathew nitakujulisha nikitoka hapa ndani” alisema Faraji na kukata simu.

“Tayari kumeanza kuchafuka.Naamini kile kilichofanyika usiku wa kuamkia leo tayari wamekifahamu. Kwa sasa tujitahidi kumuokoa Faraji Dilele ambaye jamaa wanamuwinda naye wampate. Ni yeye aliyetuwezesha tukaweza kuingia na kutumia

mfumo wa SNSA. Gosu Gosu najua umechoka lakini hakuna muda wa kupumzika. Twende haraka kumsaidia Faraji” Alisema Mathew.

MAMBO YANAZIDI KUPAMBA MOTO.

HATIMAYE GOSU GOSU AMEREJEA SALAMA KWA WENZAKE .

NANI KAMTEKA GAVANA?

NINI KITATOKEA BAADA YA BERNADETHA KUGUNDULIWA AMEUAWA?

NDUGU MSOMAJI USIKOSE SEHEMU IJAYO.